# *Mahali Pa Kuabudia Palipoandaliwa Na Mungu*

Hebu na tuinamishe vichwa vyetu kwa muda kidogo tu.

Baba mpenzi wa Mbinguni, kweli tunahesabu hii kuwa ni baraka kuwa hapa leo katika jiji hili la Los Angeles, na miongoni mwa hawa, waamini ambao . . . Wateule ambao wameitwa kutoka ulimwenguni, watoto wa Mungu waliotengwa, katika saa hii kuu tunayoishi, chini ya matarajio haya makuu ya kutokea kwa Mpenzi wetu, Bwana Yesu, wakati wo wote. Tunakushukuru kwa ajili ya jambo hili moyoni mwetu, kwamba tunaamini ya kwamba Yeye atakuja katika kizazi chetu. Tunamtarajia leo. Kama hajawasili hapa leo, na sisi tuko hapa kesho, tutakuwa tukimtarajia kesho.

2 Mungu mpenzi, tunaomba ya kwamba m—mkutano huu utakuwa tu ni mkutano maalum. Jalia iwe ni wakati ambao utavunja rekodi ya—ya ufanisi wa Kanisa, itakayokuwa kwenye Vitabu Vyako katika Umilele. Bariki kila jitihada nyonge tunayofanya, Baba. Tunatambua ya kwamba sisi hatuambui kitu kabisa bila Wewe, kwa hiyo basi ni lazima tuwe na Wewe, Bwana, kama tutaweza kuendelea. Wala hatutaki jambo hili kwa utukufu wetu wenyewe. Tunataka jambo hili kwa ajili ya utukufu Wako. Kwa kuwa hiyo ndiyo shauku yetu ya moyo, ni kumwona Yesu ametukuzwa katika watu Wake. Kuimarisha imani yao, Bwana, katika siku hii ambayo vita ni vikali sana, tumekuja kwa ajili ya ufufuo huu miongoni mwetu, na kimbilio, burudiko. Tunaomba ya kwamba utatujalia mambo yote haya; kwa kuwa tunaomba katika Jina la Yesu. Amina. Ketini.

3 Ndugu Shakarian, Dada Wyatt, na kwa marafiki wa Bwana Yesu Kristo, bila shaka ninafurahia nafasi hii ya kuwa Los Angeles tena, kumhubiri huyu Yesu mtukufu ambaye kwa sababu yake sote tumekuja hapa tupate kumjua zaidi leo. Kama jitihada zetu . . .

4 [Mtu fulani anazungumza na Ndugu Branham kuhusu maikrofoni—Mh.] Naam, bwana. [Sehemu tupu kwenye kanda] . . . aina hii. Hili ni jambo gumu sana. Aisee, kidude hiki hakitaki kuunga. [Wengine wanatoa ushauri jinsi ya kurekebisha maikrofoni.] Vema, haitafanya kazi namna hiyo. [Sehemu tupu kwenye kanda] . . . Ndugu Shakarian. Sasa hiyo inasikika afadhali zaidi.

5 Kwa namna fulani mimi ni mdogo, nina sauti ndogo, lakini basi nina Ujumbe mkuu sana kutoka kwa Bwana. Upinzani mwingi sana kutoka kwa Shetani, kuzuia nisiulete, tutafika

hapa hata hivyo. Tunatumaini hili litakuwa ni juma zuri sana kwetu sisi sote.

6 Nilikuwa nimeketi pale nikiwazia kuhusu ni mara ngapi ambapo hayati mpendwa wetu Ndugu Thomas Wyatt, bila shaka, alikuwa amehubiri kutoka kwenye mimbara ii hii, mtumishi mkuu wa Kristo.

7 Nilimjua Ndugu Wyatt. Yeye daima alikuwa akinitia moyo nilipokutana naye na kuzungumza naye. Ninakumbuka, kama tu mhubiri kijana, yeye daima angeninii. . .kitabu chake, kilichoitwa *Mbawa za Uponyaji*. Ninapenda jina hilo, *Mbawa za Uponyaji*.

8 Nasi tuna furaha kuwapo hapa kwenye hekalu hili ambalo limewekwa wakfu kwa ajili ya ibada ya Kristo. Mungu na ambariki mjane wake, na ninyi watu wote ambao. . .Hakika, ninajua mnamkosa, pia. Nilikosa kipindi chake, niliposikia ya kwamba ameaga. Nilipenda kuisikia sauti hiyo. Alikuwa anazeeka kidogo, bali angali alikuwa na sauti nzuri na yenye nguvu, na—na alikuwa ana ujumbe kutoka kwa Mungu. Na maisha yake yangali yanaishi hapa ndani yenu ninyi watu. Na huko kwenye huduma ya kimishenari alikotuma vikundi hivyo vyote, na kadhalika, Injili ingali inaendelea kwa sababu ya Thomas Wyatt. Nafsi yake na ipumzike katika amani mpaka wakati tutakapokutana naye katika ile Nchi yenye utukufu ambako hakuna mauti wala uzee. Tuko hapa kuendelea sasa mpaka wakati wetu utakapoitwa ama kwenye kiama wakati Yesu atakapokuja kutuchukua sisi sote.

9 Sasa ninajua mna ibada hapa, nafikiri, usiku wa leo. Nami niliambiwa, muda mchache uliopita, ya—ya kwamba mlikuwa na ibada hapa usiku wa leo, kwa hiyo nitaharakisha upesi niwezavyo.

10 Kwa sababu, nina Jumatatu usiku, Jumanne usiku, Jumatano usiku, na kadhalika, juma hili, kwa hiyo ninatumaini ya kwamba Bwana atatubariki. Tutawaombea wagonjwa. Tutamhubiri Kristo, kama akipenda, kama ikiwa ni mapenzi Yake, katika nguvu zote za kufufuka Kwake jinsi atakavyoturuhusu kufanya. Na cho chote atupacho kufanya, hicho tunataka kukifanya kwa moyo wetu wote. Nami ni—ninajua ya kwamba atatubariki kama tu tutamwamini.

11 Na sasa kabla tu hatujafungua Neno, kulisoma, ninataka kuzungumza Naye tena, tunapoinamisha vichwa vyetu na kutulia sasa, na tukitumaini ya kwamba matatizo yamekwisha. Tunatambua, Wakristo wote wanajua, ya kwamba adui, adui yetu, anatenda kazi kila mahali. Lakini, unaona, wakati mambo kama hayo yanapotukia, tulieni tu. Mungu anajua mambo yote. Unaona, tulieni tu, huenda Yeye alikuwa akifanya jambo fulani ambalo wewe usingejua kabisa sasa hivi. Hebu na tuzungumze Naye.

12 Baba, tunaomba sasa ya kwamba utatuliza bahari, Bwana Yesu Kristo mwenye nguvu na aje akitembea juu ya Neno Lake sasa, akituingiza, kwenye mazingira mapya, na nguvu Zake na madhihirisho. Tunaomba jambo hili, tunaposoma Neno Lake, na lihuishwe mioyoni mwetu leo, tupate kumjua Yeye, katika nguvu za kufufuka Kwake. Kwa maana tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

13 Sasa kama mtafungua kwenye Kitabu cha Kumbukumbu la Torati. Ninataka kusoma kifungu kimoja, ama viwili, kutoka kwenye Kitabu cha Kumbukumbu la Torati, mlango wa 16 wa Kumbukumbu la Torati.

> *Utunze mwezi wa Abibu,* ambao maana yake ni Aprili, *ukamfanyie pasaka BWANA, Mungu wako, kwa kuwa ilikuwa ni mwezi wa Abibu alipokutoa Misri usiku BWANA*; *Mungu wako.*
>
> *Nawe umchinjie pasaka BWANA, Mungu wako, katika kundi la kondoo na la ng'ombe, mahali ambapo atachagua*. . . (samahani) . . . *mahali atakapochagua BWANA apakalishe jina lake* hapo.
>
> *Usimle pamoja na mikate iliyotiwa chachu; siku saba utakula naye mikate isiyotiwa chachu* hapo, *nayo ni mikate ya mateso; kwa maana ulitoka katika nchi ya Misri kwa haraka:* . . . *ili upate kukumbuka siku uliyotoka nchi ya Misri, siku zote za maisha yako.*
>
> *Wala isionekana kwako chachu muda wa siku saba katika* mpaka wako wote. *mipaka yako yote; wala . . . hiyo nyama uchinjayo siku ya kwanza jioni, kisilale cho chote usiku kucha hata asubuhi.*
>
> *Usimchinje pasaka ndani ya* mlango . . . *yote akupayo BWANA, Mungu wako;*
>
> *Ila mahali atakapochagua BWANA, Mungu wako, apakalishe jina lake, ndipo mtakapomchinja pasaka jioni, katika machweo ya jua, kwa wakati kama uliotoka Misri.*

14 [Mtoto analia, katika kusanyiko—Mh.] Inaonekana kana kwamba kuna shida tena. Ninaamini ninaweza kupaza sauti kubwa zaidi kuliko huyo.

15 Ni fungu la maneno la ajabu sana ninalotaka kunena habari zake kidogo, alasiri ya leo, ni juu ya: *Mahali Pa Kuabudia Palipoandaliwa na Mungu.*

16 Sasa, hili si la kawaida. Lakini kama nilivyosema, mara nyingi hapo nyuma, ya kwamba Mungu kwa kawaida huishi katika njia zisizo za kawaida, mahali pasipo pa kawaida, hufanya mambo yasiyo ya kawaida, kwa kuwa Yeye si wa kawaida. Ye yote yule amwaminiye Yeye, hutenda isivyo kawaida. Kuna mambo mengi, mengi sana ambayo tungetaka

kusema kuhusu kutokuwa kawaida Kwake. Bali ninajua ya kwamba wote, wanaomfahamu, wanajua ya kwamba Yeye si wa kawaida, anafanya mambo yasiyo ya kawaida, mengine mara nyingi katika ule wakati usio wa kawaida. Kwa hiyo tunatumaini leo ya kwamba Mungu atabariki huku kusomwa kwa Neno, na kuhusu fungu ambalo nimechagua kuwazugumzia.

17 Sasa, kile ninachodhania kwamba kilisababisha shida yetu hapa, kilikuwa, wao walikata vinasasauti kule, na kuvuta umeme tu moja kwa moja kutoka kwenye maikrofoni. Kwa hiyo, kama hawatatengeneza hilo, mbona, mtanisikia hata hivyo. Mungu atayatengeneza maskio yetu ili tuweze kusikia.

18 Sababu ya kutaka kunena juu ya somo hili, na ni wakati mzuri wa kufanya jambo hilo, kwenye mkutano wa Wafanyabiashara wa Full Gospel, ni kwa sababu makanisa yote, ama mengi yao, yamewakilishwa katika kundi hili, madhehebu yote mbalimbali.

19 Nami ninaona, mara nyingi, ya kwamba watu, nikikutana nao barabarani, katika barabara kuu, na kwenye ndege, magari moshi, mabasi, nitawaambia, "Je! wewe ni Mkristo?"

20 Mmoja wao atasema, "Vema, mimi ni Mmethodisti. Mimi ni Mbatisti. Mimi ni Mpresbiteri. Mimi ni Mlutheri. Mpentekoste," ama kitu fulani kama hicho

21 Kila mtu ana madhehebu ambayo anataka kuwakilisha. Na hilo ni sawa kabisa kuwakilishwa na madhehebu fulani, lakini, bado, sehemu yake iliyo mbaya, kwamba kila mmoja anafikiri ya kwamba kundi hili ndilo kundi tu ambalo—ambalo litaenda Mbinguni, na ndilo kundi pekee ambalo—ambalo Mungu anawakilishwa humo, kama anawakilishwa, ni kundi fulani la mtu fulani. Nilifikiri alasiri ya leo ingekuwa ndio wakati mzuri wa kutatua jambo hilo. [Kusanyiko linashangilia—Mh.] Na labda hiyo ndiyo sababu Shetani anaendelea kushughulikia maikrofoni hii. Unajua, cho chote ambacho mwanadamu anafanya kitaharibika, bali kile Mungu afanyacho hakiharibiki. Kwa hiyo kwa kuwa ni wakati mzuri wa kufanya jambo hilo, mahali pazuri pa kufanya jambo hilo, kwa hiyo, Mungu atusaidie kwa jambo hilo, kwa neema Yake, tutajaribu kufanya vizuri sana kuzungumzia jambo hilo.

22 Sasa somo hili, linatoka katika Kitabu cha Kumbukumbu la Torati. Ninasikia ya kwamba Kumbukumbu la Torati . . . kwa kuwa nina baadhi ya Maandiko na kadhalika yameandikwa hapa.

23 Ilikuwa ni kawaida kwangu ya kwamba ningeweza kuyafikiria kwa haraka sana, bali tangu nilipopita umri wa miaka ishirini na mitano, mara ya pili, inakuwa vigumu kidogo kwangu kukumbuka yote. Kwa hiyo, ninaingia chumbani na kuomba. Na jinsi anavyonipa hayo Maandiko, ninayaandika, na labda muhtasari hapa na pale, pamoja na hayo, kwa namna

fulani kufanya akili zangu ziwazie jinsi ilivyokuwa wakati aliponipa hayo.

24 *Kumbukumbu la Torati* ni jina la Kiyunani linalomaanisha "sheria mbili," neno Kumbukumbu la Torati. Na Mungu ana sheria mbili.

25 Na moja ya hizo ni sheria ya mauti, kutotii Neno Lake. Tunaona ya kwamba, wakati Hawa alipokaidi Neno Lake, ilileta mauti. Hiyo ni moja ya sheria Zake, "Siku utakayokula, siku hiyo utakufa."

26 Na halafu ana sheria nyingine, ambayo ni sheria ya Uzima, kwa utii. Kama hufanyi *hivyo* na kadhalika, mbona, kutimiza Neno Lake, utaishi.

27 Inaishia kwenye mambo mawili, kwa namna yangu ya kuliwazia, hiyo ni, au kushika Neno Lake ama kutotii Neno Lake.

28 Moja ya sheria hizi ilitolewa Mlima Sinai. Na hiyo nyingine ilikuwa. . .Hiyo ni sheria ya mauti. Hiyo sheria nyingine ilitolewa Mlima Kalvari, ambapo sheria ya Uzima ilitolewa, kwa njia Kristo Yesu.

Yeye pia ana maagano mawili.

29 Alikuwa na Agano na Adamu, mtu wa kwanza duniani. Na agano hilo lilikuwa ni kwa masharti, "Ukifanya *hivi* na *vile*, nitafanya *hivi* na *vile*." Adamu alikuwa na jambo fulani la kufanya kusudi adumishe agano hili kuwa hai mbele za Mungu. Ilibidi atembee katika njia za Mungu, akitimiza Neno Lake lote, bila kuvunja hata Neno moja.

30 Lakini basi Yeye alifanya agano lingine, na hilo lilikuwa pamoja na Ibrahimu. Agano hili halikuwa na masharti, bali lilikuwa bila masharti. Mungu alimpa Ibrahimu agano, pasipo masharti kwake, hata kidogo. Bila masharti! Si, "Nitafanya." "Nimefanya! Tayari nimefanya jambo hilo."

31 Na hiyo ndiyo sheria ambayo Wakristo hawana budi kuishi kwayo. Si kile tunachofanya sisi wenyewe, bali ni kile alichotufanyia Yeye. Kristo amekwisha kutolewa sadaka. Si kwamba, "Atatolewa." Amekwisha kutolewa! Ni tukio lililomalizika. Yeye aliishi, akafa, akafufuka tena, akapaa Mbinguni, amerudi katika mfano wa Roho Mtakatifu. Kwa hiyo, ni kazi iliyokamilika, kwa Mungu. Kristo, asiyejua dhambi yo yote, alifanyika dhambi yangu; nipate kusimama katika nafasi Yake, Yeye alichukua nafasi yangu. Nilikuwa ndani Yake, pale Kalvari, wakati alipokufa. Hapo sina budi kufa pamoja naye, nipate kuishi. Kwa maana sheria ya dhambi na mauti iko katika mwili, huna budi kufa, upate kupatanishwa Naye.

32 Lakini sasa tunapata maneno yote haya ambayo tungeweza kutumia, masomo haya makuu, ambayo sote tunayafahamu mengi yake, na ile mifano mikuu ya Maandiko. Lakini alasiri ya

leo, tunakabiliwa na jambo hili, ya kwamba, mbele ya yote haya, Yeye angali anasema kuna mahali pamoja tu atakapokutana nawe, mbele ya nadharia zetu zote mbalimbali. Tumekuwa na dini ya Kiyahudi. Tumekuwa na Uisilamu. Tumekuwa na . . . Tuna kila namna ya kanuni za imani na madhehebu, makanisa, na kadhalika, bali hata hivyo Mungu alisema kuna mahali pamoja pekee ambapo atakutana na wewe. Mahali pote hapo, kila mmoja anasema ya kwamba, "Yeye anakutana kanisani kwangu. Na endapo wewe si mfwasi wa kanisa langu, ha—hatakutana nawe. Wewe, sharti uwe mfuasi wa kundi hili la sivyo Yeye—ama Yeye kamwe hatakutana nawe pale. Ama, hatakutana na wewe mahali pengine po pote bali pale, hasa."

33 Na halafu tunapata hapa ya kwamba Yeye ana mahali pamoja, mahali pamoja tu. "Utatoa dhabihu mahali ambapo Bwana Mungu wako atapachagua." Sasa Yeye ana mahali alipopachagua ambapo anakutana na watoto wanaoabudu, nao hawakupaswa kutoa dhabihu mahali pengine po pote bali katika mahali pamoja. Mahali pengine po pote pasingefaa kitu. Yeye alikuwa na mahali pamoja maalumu ambapo angeweza kukutana nao. Na ni mahali pamoja, pekee, ndipo anapokutana na mwabudu.

34 Basi, kama hiyo ni kweli, afadhali tuwe waangalifu sana kwamba tunapapata mahali hapo. Ninafikiri inatubidi sana, ya kwamba, sisi kama watu wanaojua ya kwamba tunakufa, na wanaoishi katika jamii inayokufa, wanaoishi katika kizazi kinachokufa, wanaoishi katika taifa linalokufa, chini ya bendera ya mauti.

35 Na ulimwengu huu hauna budi kufikia mwisho. Hauwezi kuendelea zaidi. Dhambi imefurika tele. Hauna matumaini. Hakuna matumaini tena kwa ulimwengu huu. Umepitiliza hayo.

36 Ninaamini Roho Mtakatifu anaokota masazo mashambani, akimpata *huyu* na *yule*, kwa kuwa saa imeenda sana. Injili imekwisha kuhubiriwa kwa kila taifa. Itikadi na kadhalika zimeifuata, bali hata hivyo Injili imeendelea vivyo hivyo.

37 Na sasa, kwenye wakati wa mwisho, tunaona mambo yakitendeka jinsi yanavyotendeka, kuna onyo kuu miongoni mwa wateule wa Mungu, la kupata kujua yaliyo kweli. Na inatubidi kujua jambo hilo. Sasa, si nadharia ya mtu fulani, bali ni kujua lililo Kweli, yale Biblia inayosema kwamba ni Kweli. Kwa maana, itakuwa kuna kuchelewa sana moja ya siku hizi, kwetu sisi, na huenda hii ndiyo hiyo siku, basi hebu na tutilie maanani kweli kweli kuhusu yale Mungu amesema.

38 Kumbukeni, Mungu anapotamka Neno, hawezi kulighairi kamwe. Hana budi kudumu vivyo hivyo. Hawezi kamwe kutamka jambo fulani, na kisha aseme, "Vema, si—sikumaanisha hasa jambo hilo." Unaona, Yeye hana kikomo. Anajua lililo bora kuliko yote, kwanza. Sisi husema mambo tunayodhania ni bora

kuliko yote, ndipo baada ya kitambo kidogo tunayaghairi. Bali Mungu hawezi kufanya jambo hilo, na adumu kuwa Mungu. Kwa hiyo kama hana kikomo, Yeye—Yeye hafanyi hivyo, kwa kuwa Yeye ni mkamilifu katika kila Neno. Yeye kamwe hatamki Neno lisipokuwa ni la Milele. Mambo Yake yote ya Milele yalikuwa pamoja Naye hapo mwanzo, mawazo Yake, sifa Zake, na zinajidhihirisha tu zenyewe ulimwenguni leo.

39 Sasa, kumbuka, Yeye ana mahali alipopaandaa, mahali pamoja pekee ambapo atakutana na watoto waaminio. Mahali pengine po pote hapatafaa kitu.

40 Kumbuka, Yesu alisema, alipokuwa hapa duniani, akizungumza na kundi la watu ambao walikuwa ni wa kidini sana, watu wazuri sana, wastaarabu sana, watu wenye bidii sana, na Mungu, lakini Yesu aliwaambia, "Mnaniabudu bure," kufundisha Fundisho lao lililo mapokeo ya binadamu. Kumbuka jinsi watu hao walivyokuwa wachaji, na jinsi walivyokuwa na bidii ya Mungu. Ninaamini kama tulikuwa tukiwahesabu watu ambao walikuwa na bidii zaidi, wa siku hizi ama siku zile, wangekuwa na bidii zaidi kuliko sisi. Kwa mbali zaidi! Ilipofikia kushika mapokeo na sheria, na kadhalika, waliishi kwa hayo. Nao walikuwa na bidii sana na Mungu, na walimwamini Mungu. Lakini Yesu, Mungu aliyefanyika mwili miongoni mwetu, alisema, "Mnaniabudu bure." Sasa, Yeye hakusema kwamba hawakumwabudu. Walikuwa wakimwabudu, bali bure.

41 Kwa hiyo cho chote kilicho bure hakina, hakina faida, hakifai hata kidogo. Hupaswi kukifanya kamwe, kwa sababu unapoteza tu wakati wako. Unapoteza pumzi yako, unapoteza jitihada zako, mpaka tutakapofikia kujua kile tunachofanya.

42 Hakika ikiwa Mungu anawatarajia watu kuwa wakamilifu, kama Yesu alivyosema, "Basi ninyi mtakuwa wakamilifu, kama Baba yenu wa Mbinguni alivyo mkamilifu," inabidi kuwe na matayarisho fulani mahali fulani. Naye alisema, "Nitapachagua mahali ambapo watu wataniabudia. Sitakutana nao mahali pengine po pote." Na, sasa, hapana budi pawe ni mahali hapo, nasi tunapaswa kupatafuta. Tutafute ni wapi, kisha twende pale. Ninafikiri tunapaswa kuelekea kule, haraka, tutakapopapata mahali hapo, tukiachana na mambo mengine.

43 Sasa, kumbuka, Yesu alisema katika Andiko lili hili hapa ambalo ninanukuu. Mapokeo ya wanadamu basi ni bure. Haitupasi hata kidogo kujipumbaza nayo. Inapaswa kuwepo, na mahali fulani, mahali fulani ambapo Yeye ametuandalia sisi, ambapo tungeweza kuja na ibada hiyo ikubalike. Sasa, kumbukeni, nje ya mahali hapo palipochaguliwa, haidhuru u mwaminifu jinsi gani, jinsi ulivyo mfuasi wa kanuni za kimsingi, ungali unaabudu bure.

44 Ninajua hilo linasikika ni la kikatili. Bali, lile jengo liko karibu na kumalizika, hatutaki litikisike. Hebu na tulifunge kwa

Injili, ili kwamba watu wakikutana nanyi mitaani, ama po pote mlipo, ninyi Wakristo, iwe kwamba mtakuwa na la kuwajibu.

45 Katika wakati ambapo wao wanasema, “Loo, *hili* ni Lile. Nami nimeona *hawa* wakifanya hili, na *wale* wakifanya lile.” Bila shaka, mambo haya yote hayana budi kutukia. Bali kuna mahali ambapo pametolewa na Mungu peke yake, na hapo ni mahali pale ambapo Mungu hukutana na mwabuduo, peke yake.

46 Angalia kifungu cha 2, “Kuabudu katika mahali nilipopachagua.” Palipochaguliwa kwa ajili gani? Mahali hapa panaonyesha, ya kwamba Yeye yuna mahali ambapo watu wote huabudu. Mahali pengine ni bure. “Na katika mahali hapa,” Yeye alisema, “Nimepachagua pia kuweka Jina Langu katika mahali hapa. Nitachagua mahali, Nami nitaweka Jina Langu ndani yake, mahali hapa ambapo mtu ataabudia.”

47 Sasa, hii inaonyesha ya kwamba kuna mahali pamoja, mahali pamoja tu. Panapaswa pawe ni chaguo la Mungu; hapawezi kuwa ni letu. Hatuna chaguo la kufanya; Yeye tayari amepachagua. Sasa, kile Mungu anachochagua ni sahihi. Mimi ninaweza kuchagua vibaya, wewe unaweza kuchagua vibaya, bali Mungu hawezi. Anachagua sahihi. Hata hivyo, ni, Yeye ndiye anayeabudiwa. Naye ana mahali ambapo anawataka waabuduo Wake wakutane pale, nasi tunapaswa kukutana Naye pale. Hapo ndipo mahali pekee ambapo Yeye anakaa; mahali pekee ambapo atakusikia kutoka hapo.

48 Hebu na tuone hapa, pia, “Mahali nilipopachagua niabudiwe hapo, nitaweka Jina Langu mahali hapo.”

49 Loo, sasa hebu na tuyachunguze Maandiko kwa ajili ya mahali hapo ambapo amepaweka Jina Lake. Sasa tuna vivuli na mifano, kote katika Biblia, tunajua hivyo, kuhusu mahali mbalimbali ambapo Yeye alikutana na watu, bali hapo si mahali ambapo Yeye atakutana nao siku hizi. Kwa maana zilikuwa tu zikionyesha kivuli cha kitu fulani, kilichoelekeza kwenye mahali halisi ambapo Yeye atakutana na watu hao, mahali hapo, Kanisa ambalo atakutania hapo. Na kuna mahali pamoja, kuna Kanisa, ambalo Mungu aliahidi kukutana na watu mahali hapa na kujibu maombi yao, kama tu wangekuja mahali hapa na kumwabudu.

50 Sasa tunaona ya kwamba kuna wengi wanaodai ya kwamba—ya kwamba wao wanapo mahali hapo, Jina la Mungu lipo katika mahali pao. Lakini, unaona, *wao* waliliweka Jina la Mungu pale. Kuna tofauti kubwa kati ya Mungu kuweka Jina Lake pale, na mtu fulani kuliweka pale, Jina Lake hapo. Unaona? Lazima tukumbuke kwamba Mungu alisema, angeweka. “Nimeweka Jina Langu. Nitaliweka Jina Langu mahali hapa. Na hapo ndipo mahali ambapo napachagua, na nimepachagua, ambapo watu wanapaswa kuabudia.”

51 Jambo hili, linatuleta sasa mbele ya vivuli hivi vya wakati, hutuletea Kristo mbele ya macho yetu. Agano lote la Kale lilionyesha kivuli cha Yesu. Huko Misri, usiku ule ambapo kulikuwa kuwe na mwana-kondoo wa pa—pasaka aliyeuawa kwa ajili ya ulinzi wa watu, tunatambua ya kwamba Mungu alikuwa na mahali pamoja, sharti moja. Haidhuru ni kijana jinsi gani, kuhani alikuwa ni mzee jinsi gani, kasisi, cho chote ulichokuwa, unapaswa kuwa katika mahali fulani hapa. Wote waliokuwa nje ya mahali hapo, waliangamia. Unapaswa kuwa katika mahali hapa pamoja, mahali ambapo Yeye alipaandaa.

52 Sasa, tungeweza kutumia wakati mwingi, alasiri ya leo, katika kuelezea jambo hilo, ambapo ingekuwa tu ni kurudia yale tunayojua tayari, jinsi ambavyo Kristo alitangulia kuonyeshwa katika vivuli kivuli na mifano. Yule Mwana-Kondoo wa sadaka, jinsi anavyopaswa kuwekwa, dume asiye na waa, na jinsi anavyopaswa kuuawa na wazee, na jinsi ambavyo kwamba damu inapaswa kunyunyiziwa kwenye mlango, yote yakionyesha mfano wa kuja Kwa Kristo. Na chini ya damu hii iliyomwagika palikuwa ni mahali ambapo Mungu alikutana na mwabuduo, wakati ambapo malaika wa mauti alipitia nchini.

53 Ninaamini ya kwamba tuko tayari kutoka Misri, moja ya siku hizi, na kuingia katika Nchi hii ya ahadi. Na wakati umewadia wa kuingia mahali palipo sahihi, na kuacha huku kuzozana, "Mimi ni Mpresbiteri. Mimi ni Mmethodisti, Mimi ni Mbaptisti. Mimi ni *hili*. Mimi ni *lile* ama *linginelo*." Tokeni kwake, na mpatafute mahali hapa ni wapi, kwa kuwa mauti yako kila mahali mbali na mahali Pake alipopachagua. Mauti itapiga kwa hakika kabisa, endapo hatupo katika mahali Pake alipopachagua. Bali mahali anapopachagua, mauti hayawezi kuja.

54 Kama ukiangalia katika mwana-kondoo wa sadaka, mauti yalikuwa tayari yamezuru pale. Mauti ilikuwa imekuja mahali hapa kwa kuwa mwana-kondoo huyo alikuwa amekufa. Mauti yalikuwa tayari yamezuru. Na kwa hiyo mahali ambapo mauti yalikuwa yamezuru, ndipo Mungu aliahidi ya kwamba Mahali hapo pangekuwa ni Pake. Basi, tukimwangalia, tunaona jinsi yule mwana-kondoo wa sadaka alivyokuwa, kwamba mahali pa uzima palikuwa ni wapi wakati huo.

55 Sasa, kwangu mimi, hili linakatilia mbali ubishi wote. Tukiwa tunamwona Kristo, akiwa Mwana-kondoo wa sadaka, basi hilo linakatilia mbali madhehebu yote, kanuni zote za imani, mafundisho yote ya sharti, ukanisa wote. Linakanusha jambo hilo lote. Hiyo ni kweli, kwa kuwa tunamwona, hapa, Yeye waziwazi, kwa kuwa Yeye ni Neno safi lisiloghoshiwa la Mungu. Yohana Mtakatifu 1, ilisema, "Hapo mwanzo kulikuwako Neno, neno alikuwako kwa Mungu, naye Neno alikuwa ni Mungu. Naye Neno alifanyika mwili akakaa kwetu." Kwa hiyo yeye ni Neno la Mungu lisiloghoshiwa lililofanyika mwili, lililodhihirishwa.

56 Na hili likiwa linaonekana wazi, tusingeweza kuliweka hilo kwenye kanisa lo lote ulimwenguni leo, madhehebu yo yote. Mahali po pote kama hapo, tusingeweza kuliweka, kwa kuwa sivyo ilivyo. Tunaweka Jina la Kristo kwenye jengo fulani, tunaliita makanisa ya "Kristo," na *hili*, *lile*, ama *lingine*. Hilo halilifanyi kuwa ndivyo lilivyo. Hilo halitimizi jambo hilo, hata kidogo. Bali wakati Mungu anapoweka Jina Lake katika jambo fulani, hilo ndilo linalotakiwa.

57 Sasa, hakuna kitu kwenye Biblia ambacho kingekuwa ni mfano wa madhehebu yetu ya kisasa, ila Babeli. Huo ndio mfano wa pekee katika Biblia wa madhehebu yetu ya kisasa, dini ya kimadhehebu, kwa kuwa ilianzishwa na Nimrodi na umoja wa kulazimishwa miongoni mwa watu wa kidini. Na hivyo ndivyo kanuni za imani na madhehebu yetu yanavyofanya leo, kulazimisha umoja, "Ama uwe ni mfuasi wa hili la sivyo uko nje!" Na tunakuja sasa, kama tunavyoweza kuona, kwenye kulazimishwa kwa wote katika umoja mmoja mkuu wa kitu hicho. Bali hicho ni chombo kilichotengenezwa na binadamu, wala hakiwezi kusimama. Si mapenzi ya Mungu. Si mpango wa Mungu, haidhuru ni vipi watu wanajaribu kusema ndivyo ulivyo. Sivyo ulivyo. Haiwezekani. Haliwezekani kabisa, huo kuwa. Mungu asingeweza kuweka Jina Lake katika kitu kama hicho kinacholikana Neno Lake. Mungu anawezaje kuishi katika kitu kinachokana Neno Lake Mwenyewe? Huwezi kufanya hivyo.

58 Kwa hiyo tunaona, halikai kwenye kanisa lo lote, Methodisti, Baptisti, Presbiteri, Pentekoste, Katoliki, Orthodoksi ya Kiyunani, lo lote lile. Si mahali pa Mungu pa kuabudia, bado.

59 Sasa hebu tumwache Mungu, aliyetoa ahadi hii, ajitokeze na kuithibitisha, kwamba ni kweli. Hiyo ndiyo jinsi ya kufanya jambo hilo. Kama Yeye angali ni Mungu, Yeye angali ni Mungu! Kama alipata kuwa Mungu, anabaki kuwa Mungu!

60 Na sasa tunaona hii dini ya kulazimishwa, ikionekana wazi kabisa sasa, kuleta vikundi vyote vidogo katika "umoja mkubwa mmoja," wanavyouita. Baadhi yao wanaamini katika *hili*, na wengine wao wanaamini katika *lile*; na wengine wanakana jambo *hili*, na wengine wanakana jambo *lile*. Biblia ilisema, "Watu wawili wanawezaje kutembea pamoja wasipopatana?" Halitawezekana kamwe.

61 Inatupasa kupatana. Na ni kupatana katika nini? Si kupatana mmoja kwa mwingine, hata ingawa inatubidi kupatana na Neno, na Mungu. Hilo ndilo tunalopaswa kupatana nalo.

62 Sasa tunaona, na umoja wa kulazimishwa uliwakilishwa na makundi ya watu huko Babeli. Mungu hawezi kuweka Jina Lake katika kitu kama hicho. Hajapata kuliweka wala hataliweka kamwe. Ingawa walijaribu, waliweka jina lao mle, waliweka Jina Lake mle, bali sivyo ilivyo.

63 Bali ni lazima tutafute mahali alipoweka Jina Lake, kwa maana hapo ndipo mahali na mahali pekee ambapo Yeye amewaandalia Wakristo kuja, na watoto wanaoamini, na kumwabudu Yeye mahali hapa. Je! mahali hapa pangekuwa ni wapi?

64 Sasa kuunga jambo hilo mkono, tungeweza kuchukua Biblia nzima kuunga mkono yale ninayoenda kusema. Kwa kuwa, mahali ambapo Yeye alichagua pako katika Kristo, katika Yesu Kristo. Ni katika Yeye, Mwanawe; Mwana wa Mungu, Yesu Kristo.

65 "Vema," ulisema, "Nilifikiri Maandiko yanasema hapa ya kwamba Yeye alisema angepachagua mahali hapo na angeweka pia 'Jina' Lake katika mahali hapo."

66 Vema, mwana daima huchukua jina la baba yake. Jina langu ni Branham kwa maana baba yangu alikuwa ni Branham.

67 Na Yesu alisema ya kwamba alikuja katika Jina la Baba Yake. Yohana Mtakatifu 5:43, "Nilikuja katika Jina la Baba Yangu wala ninyi hamnipokei," kwa hiyo hapo ndipo Mungu alipoweka Jina Lake, chini ya dhabihu ya Mwanawe Mwenyewe! Hapo ndipo mahali pekee Mungu alipoandaa. Hapo ndipo watu wanapoweza kukutana na Mungu, ni katika Kristo. Hapo ndipo mahali Pake alipoandaa. Hakuna madhehebu, hakuna kanuni za imani, hakuna kitu kingine cho chote, Mungu ameahidi kukutana. Atakutana tu katika Yesu, kwa kuwa hapo ndipo mahali pa pekee palipo na Jina Lake.

68 Pia tunamsikia Yesu, ninapofuatilia Maandiko, Yohana, Yohana mlango wa 5 na kifungu cha 43, Yeye alisema, "Mwingine atakuja, na aje katika jina lake, na huyo mtampokea." Tunaweza kujiunga na kanuni ya imani, "mwingine," tunaweza kujiunga na madhehebu, mtampokea; bali wakati unapompokea Yesu, ni tofauti. "Mwingine atakuja, 'Nitasema mimi ni Mmethodisti, mimi ni Mbaptisti, mimi ni Mpresbiteri,' mtampokea huyo vizuri. Bali nimekuja katika Jina la Baba Yangu, nikitenda yale Baba aliyosema ningetenda, wala hamnipokei." Akasema, "Yohana alikuja, naye alikuwa na ushahidi mkuu, bali Mimi nina ushahidi mkuu zaidi katika Mungu—katika Mungu kuliko vile Yohana alivyokuwa nao. Kwa maana yale Baba aliyonipa kufanya, hayo ninafanya," Maneno yaliyoandikwa juu Yake, kile anachopaswa kuwa katika siku hiyo. Kwa kuwa Yeye alikuwa . . .

69 Jina Lake lilikuwa ni Mungu. Mungu ana vyeo vingi. *Mungu* ni cheo, Chenyewe, aliitwa Yehova-Yire, Yehova-rafa, Yehova-manase. Aliitwa Ua la Uwandani, Ninyoro ya Bondeni, Nyota ya Asubuhi; Alfa, Omega, Mwanzo na Mwisho; halafu Baba, Mwana, Roho Mtakatifu; vyeo hivi vyote.

70 Bali Jina Lake, Jina la Mungu ni "Yesu Kristo," Aliyetiwa Mafuta. Hilo ndilo Jina Lake. Alikuwa na vyeo vingi, bali Jina moja, la pekee, "Hakuna Jina lingine chini ya Mbingu

walilopewa wanadamu, ambalo unapaswa kuokolewa kwalo." Tunaona ya kwamba hiyo ni kweli.

71 Pia onyo hili, ya kwamba, "Wakati huyu mwingine atakapokuja, ya kwamba alikuja katika jina lake mwenyewe, 'Methodisti, Baptisti, Presbiteri, Pentekoste,' kadhalika, mtampokea. Mtajiunga naye." Bali Kristo anakataliwa. Wanamkataa Huyo.

72 Nabii alisema! Hebu na tulifuatilie jina lake kidogo. Nabii alisema, "Ataitwa Jina Lake 'Imanueli.'" Sasa, Isaya alisema hilo, kwenye mlango wa 7 hivi. Na pia katika Mathayo 1:23, alisema, "Hayo yote yalikuwa ili litimie neno lililonenwa na Bwana kwa ujumbe wa nabii, akisema, 'Ataitwa Jina Lake *Imanueli*, ambalo tafsiri yake ni "Mungu pamoja nasi."'"

73 Imanueli, na Jina Lake lilikuwa ni Yesu, Mungu pamoja nasi, akiwa na Jina la Baba Yake. Alikuja katika Jina la Baba Yake. Hapo ndipo Mungu alipoweka Jina Lake, katika Mwanawe. Hapo ndipo mahali pekee unapoweza kumwabudu. Mahali pekee Mungu atakapokutana na Wewe, ni katika huyo Mwana ambaye alifananishwa na mwana-kondoo wa sadaka. Na huko nyuma kote katika Agano la Kale, kote kulileta mifano ya jambo hilo moja, ya kwamba mahali hapo peke yake, Mungu, hapo pekee, ndipo alipokutana nao chini ya damu ya sadaka. Mahali pekee alipokutana, ndipo mahali pekee anapokutana leo; si katika jina la kanuni ya imani, ama jina la madhehebu, jina la kanisa, wala jina la kundi fulani, ama jina la shirika fulani, bali ni katika Jina la "Yesu Kristo!"

74 Nilionja hilo wakati nilipokuwa kijana mwanamume. Mara kwa mara nilikuwa nimesikia juu ya mizimu, juu ya Ibilisi, jinsi anavyofanya mambo. Nami nilijua kama kulikuwako na Mungu, hapana budi kuwepo na Ibilisi, kwa maana Biblia ilisema Ibilisi alikuwapo. Naye, nilifikiri...nilisikia juu ya hawa vijumbe. Nilienda kwa baadhi yao, nikakuta kwamba walikuwa ni bandia, hakuna cho chote, ni kundi kubwa tu la vijumbe bandia. Bali nilikuta kwamba kulikuwa na baadhi yao waliokuwa ni vijumbe halisi.

75 Nami nilikuwa katika kambi moja wakati mmoja, ambako mimi na mhudumu fulani tulienda kuwaona kule waliko. Walikuwa wameinua meza kutoka sakafuni, iliyokuwa na gilasi za wiski juu yake; na wakachukua meza hiyo, wakaipindua huku na huku. Na gita lilikuwa likipepea humo chumbani; nguo za watu. Walikuwa wameiinua hii juu, humo chumbani. Kasema, hiki kijumbe kikasema, "Nampa changamoto mtu ye yote kuiangusha chini sakafuni."

76 Wanaume wawili walisema, "Nitaishusha." Wakaishika kwenye miguu namna *hiyo*, na kujaribu kuishika. Haikushuka. Mbona, meza hiyo iliwatupilia moja kwa moja chini upande wa pili wa chumba.

77 Usiketi karibu na hapo. Kama hujawahi kuwa mmishenari na kufanya huduma huko, jambo pekee ujualo ni wazo tu la Ibilisi fulani. Kama ukiangalia hapa nje katika baadhi ya watu hawa wanaotembea mitaani, unaweza kumwona. Lakini Ibilisi yuko! Hakika yuko.

78 Na watu wanamwabudu Ibilisi, hata hawajui wanalofanya. Wanamwabudu Ibilisi makanisani, "Wakifundisha Fundisho lililo maagizo ya mwanadamu, kanuni—kanuni za imani na mapokeo." Nilisema . . .

79 Mwanamke huyu alinipigia makelele, na kusema, "Wananiambia ya kwamba wewe ni mhubiri."

Nikasema, "Ndiyo."

80 Akasema, "Basi kama huninii . . . " Kasema, "Unasemaje juu ya jambo hili?"

Nikasema, "Ni Ibilisi."

81 Naye akasema, "Vema basi, kama wewe una nguvu nyingi hivyo, iangushe chini."

82 Nikasema, "Mimi sina nguvu zo zote, hata kidogo. Sina nguvu, bali niko hapa nikimwakilisha Mmoja."

83 Nikasema, "Bwana Yesu, Wewe ulisema, katika Marko Mtakatifu mlango wa 16 'Katika Jina Langu watatoa pepo.'" Nikasema, "Sasa, ili kwamba mtumishi Wako apate kujua, kwa kuwa vita viko mbele yangu!"

84 Nikasema, "Ninaamuru meza hiyo ianguke, katika jina la 'Kanisa takatifu,'" nayo ilikaa pale pale. Nikasema, "Ninaamuru meza hiyo ianguke hapo chini, katika jina la 'Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu,'" ilikaa pale pale. Nikasema, "Ninaamuru meza hiyo ianguke chini, katika Jina la 'Yesu Kristo,'" basi karibu ivunjike miguu yote minne, ilipoanguka chini!

85 "Katika Jina Langu watatoa pepo!" Hilo ndilo Jina la Baba. Yeye aliweka Jina Lake katika Yesu Kristo. Na ndani Yake Yeye anakutana, kuabudu. Ndani Yake anakutana, kutoa pepo. Ndani Yake anakutana, kuponya wagonjwa. Ndani Yake anakutana, kuokoa. Ndani Yake anakutana, kuokoa, kujaza na Roho Mtakatifu. Hapo ndipo mahali pekee pa kukutana na watu kwa ajili ya kuabudu. Sasa tunaona ya kwamba Yesu alisema pia ya kwamba . . . Neno, Jina *Yesu*, limaanisha "Yehova-Mwokozi," Yehova Mwokozi.

86 Kumbukeni, "Hamtamwabudu Bwana . . . " Kwa nini? Kifungu cha 5, "Hamtamwabudu Mungu katika malango yo yote, ambayo Bwana Mungu anawapa. Malango yo yote, hamtamwabudia hapo," Mungu alisema, katika kifungu cha 5 hapa, cha Kumbukumbu la Torati 16. "Hamtamwabudia kwenye malango yo yote, ambayo Bwana Mungu anawapa. Yeye aliwapa mambo haya kwa ajili ya majaribu." Tutaingia kwenye jambo hilo, juma hili, Bwana akipenda, tuone kama Mungu hughairi

Neno Lake, ama haghairi. Angalia, Yeye aliwapa haya malango, bali msimwabudu Bwana kwenye yo yote ya malango hayo, kwa kuwa Bwana Mungu wenu hatakutana nanyi pale.

87 Bali Bwana Mungu amechagua lango. Amechagua mlango. Yesu alisema, katika Yohana Mtakatifu mlango wa 10, "Mimi Ndimi mlango wa kondoo. Mimi Ndimi huo mlango." Yeye ni Yehova-Mwokozi.

88 Sasa tungeweza kuendelea hapa kwa saa nyingi, tukielezea jambo hilo. Lakini nina hakika mnafahamu jambo hilo, kwa matendo yenu, kwamba m—mnaitikia Kweli na Neno. Kwa hiyo hatutaendela mbele zaidi, unaweza kulipeleka po pote utakapo. Kila mahali unapokuja, kama ni Kweli, litarejea moja kwa moja liafikiane na Neno lingine lote. Huwezi kuifanya Biblia iseme jambo moja mahali pamoja, na jambo lingine mahali pengine, ni kinyume cha yale aliyosema kwanza. Halina budi kuwa vile vile wakati wote.

89 Ninaacha Maandiko mengi hapa juu ya jambo hili, kwa sababu tu ninaona muda umeenda. Na dada yetu na hao wengine watakuwa na ibada hapa usiku huu, na tunataka kuwaombea wagonjwa. Hiyo ni kusema, na hebu angalia, Billy, kama wana kadi za maombi.

90 [Mtu fulani anasema, "Hakuna ibada usiku wa leo."—Mh.] Hakuna ibada. Vema. Vema, vema. Sawa. Sasa hebu na tupatafute. Sawa. Sawa. [Kusanyiko linashangilia] Tunatumaini ya kwamba Bwana atambariki bibi huyu kwa ajili ya jambo hili, kuturuhusu kutumia mahali hapa, kutupa wakati huu.

91 Kuna mathibitisho mengi sana yasiyokanushika ya kwamba Yesu ndiye mahali hapo. Yeye ndiye lango. Yeye ndiye lile Jina, na njia pekee iliyoandaliwa ambapo Mungu anapo pa kukutana na mwanadamu katika ibada. Yeye ndiye Njia, Kweli, na Uzima; Lango, Mlango; Alfa, Omega, Mwanzo na Mwisho; Ua la Uwandani, Ninyoro ya Bondeni, Nyota ya Asubuhi; Alfa, Omega. Yeye ni yote, yote yale yakiwekwa pamoja. Yeye ni Shina na Mzao wa Daudi pia, Nyota ya Asubuhi ing'aayo. Ndani Yake mnakaa utimilifu wote wa Uungu, kwa jinsi ya mwili, ambapo sisi ndani humo ni wana na binti za Mungu, katika Uungu wa Mungu. Naam. Kama wana na binti, tuko katika familia, kama wewe umo humo ndani.

92 Sasa tunaingiaje katika mahali hapa pakuu kuabudu? Hilo ndilo swali linalofuata. Tunaingiaje katika mahali hapa, kama Yesu ndiye mahali hapo? Yeye ndiye Jina la Mungu. Yeye ndiye mahali pa Mungu pa kuabudia. Naye ndiye mlango wa pekee kwa zizi la kondoo. Basi tunataka kuona jinsi tunavyoingia ndani Yake basi.

93 Sasa, kama ukiingia kwenye mlango, bila shaka, unaingia kama familia, kama tulivyokuwa tukizungumza hivi majuzi kuhusu hayo, ninii . . . ama kwenye kiamshakinywa, juu ya yule

kondoo mdogo, kwamba Mungu asingefunga mlango mpaka atakapompata yule kondoo mdogo wa mwisho na kumwingiza. Kama umeingia, basi unakuwa familia. Wewe ni familia ya Mungu unapoingia ndani ya Mungu. Bali huwezi kuwa familia ya Mungu na uwe Mpresbiteri, Mmethodisti, Mbaptisti, na Mpentekoste. Huwezi kufanya jambo hilo. Inakubidi kuingia katika Yesu Kristo.

94 "Vema," unasema, "tulifanya hivyo." Tutaona kama mlifanya hivyo.

95 Hebu na tuone vile Biblia inavyosema sasa. Tunaona, katika Wakorintho wa Kwanza, sura ya 12, Biblia ilisema, "Kwa Roho mmoja sisi sote tumebatizwa kuwa Mwili mmoja." Tumebatizwa katika Mwili wa Kristo, kwa Roho Mtakatifu mmoja. Hatuingizwi kwa kupewa mkono, hatuunganishwi, hatubatizwi kwa maji tupate kuingizwa. Tunabatizwa kwa Roho Mtakatifu, ndani ya Mwili wa Yesu Kristo.

96 Inadumu muda gani unapoingia Mle, hata utakapotenda mabaya? Waefeso 4:30 inasema, "Msimhuzumishe Roho Mtakatifu wa Mungu, ambaye kwa Yeye mmetiwa muhuri hata siku ya ukombozi wenu." Hebu bishana Naye, si na mimi. Hivyo ndivyo linavyosema. Ninalisoma. Sawa. "Unatiwa muhuri hadi siku ya ukombozi wako," hata siku Yesu atakapokuja kwa ajili yako. Basi wazia jambo hilo!

97 Ndipo wewe si wewe tena, u kiumbe kipya, kwa maana Kiyunani hapo kinamaanisha "uumbaji mpya." Umeumbwa upya tena. Nguvu za Mungu zinashuka juu yako, nawe unakuwa kiumbe kipya kilichoumbwa; jambo ambalo linaleta utu wote, utu wa kiroho na kila kitu, chini ya mamlaka ya Neno la Mungu. Wala hauna njia nyingine!

98 Unawezaje kusema ya kwamba wewe ni Mkristo, na ukatae kutii Neno Lake katika jambo moja? Ye yote aliyekataa kutii torati katika moja—sehemu Yake moja, alikuwa na hatia ya yote. Mtu ye yote! Yesu alisema, "Mtu hataishi kwa mkate tu, bali kwa kila Neno litokalo katika kinywa cha Mungu." Si sehemu tu ya Neno; kila Neno! Hayo aliyasema katika Ufunuo 22. "Mtu ye yote atakayeondoa Neno moja kutoka katika Kitabu hiki, au kuongeza neno moja Kwake, sehemu ya—yake itaondolewa kutoka katika Kitabu cha Uzima." Haitupasi kuondoa kutoka katika Biblia, wala kuongeza Humo. Sema tu vile lisemavyo.

99 Na katika Wakorintho wa Kwanza 12, lilisema, "Kwa Roho mmoja sisi sote tumebatizwa kuwa Mwili mmoja."

100 Sasa baada ya wewe kuwa katika Mwili huu, Warumi 8:1 ilisema, "Sasa, basi, hakuna hukumu ya adhabu juu yao walio katika Kristo Yesu, wasioenenda kwa kufuata mwili, bali kwa kufuata Roho." Hapo ndipo mahali ambapo hapana adhabu ya hukumu. Kama unaenda kwenye kanisa la Methodisti, Baptisti, Presbiteri, po pote lilipo; kama uko katika Kristo, wewe ni

kiumbe kipya, wala hakuna hukumu ya adhabu ndani yako, po pote pale hata kidogo. Hapo ndipo mahali pa Mungu pa kukutania. Hapo ndipo Mungu anapokutana na mwabudu. Hapo ndipo unapohesabiwa kuwa ni kiumbe kipya, kwa kuwa wamekufa kwa mambo ya ulimwengu. Wako hai katika Yeye. Uwepo ulio hai wa Mungu uko pamoja nao, siku kwa siku.

101 Yeye anaishi ndani yao, katika kila kizazi. Kila kizazi kilichokuja, kote katika Biblia, wakati mwanadamu anapotimiza masharti ya Mungu, anakuja mahali ambapo Yeye alipaandaa katika Neno Lake lililoandikwa kwa ajili ya siku hiyo, Mungu anamfanya mtu huyo kuwa ni kiumbe kipya, wala hana hukumu ya adhabu. Mwangalie Ayubu.

102 Je! ninawaumiza maskio, jinsi ninavyoongea kwa vipaza sauti hivi? Samahani. Ninajua ni kule kurudisha mwangwi hapa. Ninausikia hapa, mimi mwenyewe.

103 Lakini, angalia. Ayubu, haidhuru ni watu wangapi wanajaribu kumlaumu, ni wangapi waliosema ya kwamba alikuwa amekosea, yeye alikuwa akitimiza amri ya Mungu, kwa ile dhabihu ya kuteketezwa. Alijua ya kwamba alikuwa amehesabiwa haki, kwa maana alikuwa akizishika amri za Mungu. Hivyo ndivyo alivyohesabiwa haki, kwa sababu alikuwa akifanya mambo ambayo Mungu alimtaka ayafanye.

104 Uwepo wa Mungu ulio hai unaangaza siku hizi, kila siku, kutoka kwenye mauti ya kanuni za imani, hadi kufikia kwenye Uzima na Neno la siku hii. Sasa, Mungu ana mambo anayotenda.

105 Kama u—ua dogo, kama nilivyosema hivi majuzi asubuhi kwenye kiamshakinywa. Mbegu inapofikia kwenye nuru, inaanza kukua. Inakunywa kutoka kwenye chemchemi ya Mungu, inaendelea kukua mpaka inafikia kwenye sehemu ya chipukizi, inafikia kwenye ua, hadi kufikia kuchanua.

106 Sasa tunaona, ya kwamba tunapoanza na Kristo, tunakua namna ile ile, kwa kuwa tunakua katika neema na katika marudio ya Mungu.

107 Mpango pekee ulioandaliwa na Mungu, kwa ajili ya kizazi cho chote, ni Neno Lake. Mwanawe alikuja na akadhihirisha kila ahadi iliyoahidiwa kwa ajili ya wakati Wake. Manabii wote walikuja sawasawa kabisa katika wakati wao, wao walikuwa ni Neno la Mungu likiishi duniani. Walikuwa ni Neno. Yesu alisema ya kwamba walikuwa ni "miungu." Yesu aliita manabii hao, "miungu."

108 Mtu fulani alikutana na mimi katika ule mkutano wa mwisho niliokuwa nao, alisema, "Wewe ni mwanatheolojia duni."

109 Nami nikasema, "Mimi sidai kuwa ni mmoja." Nikasema, "Neno halimjii mwanatheolojia; yeye hujiliwa na theolojia." Neno huja . . . Unaona? Nikasema, "Theolojia tu ndiyo inayomjia

mwanateolojia. Lakini," Nikasema, "tunazungumzia juu ya jambo lingine."

110 Sasa tunaona ya kwamba, katika kila kizazi, wakati Mungu aliposema jambo fulani lingetukia, jambo ambalo lingetukia, huyu hapa mtu huyo anajitokeza na kudhihirisha hilo, hawa hapa watu wao wanajitokeza na kuliishi hilo. Huyo alikuwa ni Mungu Mwenyewe akiishi ndani ya watu hao, kwa sababu lilikuwa ni jibu la Neno Lake.

111 Sasa, njia pekee iliyoandaliwa na Mungu na mpango wa kipekee, leo, ni Mwanawe, kupitia kwenye Neno Lake kwa ajili ya wakati huu, likihuishwa na Roho ya uhai Wake, likihuishwa.

112 Sasa tuna shule maarufu za teolojia. Na mara nyingi tunapofanya jambo hilo. . . Hakuna kitu dhidi yake, hakika hakuna. Bali, unaona, unapokuwa na shule ya teolojia . . .

113 Yesu alisema, katika Yohana Mtakatifu 4, "Wakati unakuja, na sasa upo, wakati Mungu, akiwa ni Roho, ataabudiwa katika Roho na katika Kweli." Sasa watu wengine wana Roho, bila Kweli. Wengine wana Kweli, bila Roho.

114 Kwa hiyo ni kama tu kama tungalikuwa na gari kubwa, tulikuwa tukisafiri kuelekea mahali fulani kwa Kadilaka. Na Kadilaka hizo mbili zilikuwa zinafanana kabisa, nasi tulizisukuma kuzitoa hapa nje na tukaninii . . . kuzipandisha juu hadi kwenye matangi, na zote mbili tukazijaza na petroli. Nawe unapiga na kupiga moja hendeli. Vema, unaangalia, unasema, "Kiti kiko sawa. Usukani ni mzuri sana, una vinundu vya almasi. Na ni safi sana, unakaa . . . umekaa vizuri. Nawe unaketi huko nyuma na kulala. Na, loo, mambo mengi sana ungaliweza kufanya, kila kimoja, lakini, unaona, moja ya hizo . . . Zote zina mitambo sahihi, bali moja ya hizo ina dainamikia. Unaona, unaweza ukajua mitambo, bali inahitaji dainamikia kuanzisha mitambo, kuifanya itende kazi.

115 Na hiyo ndiyo shida ya kanisa siku hizi. Tumejaa teolojia, bila dainamikia yo yote ndani yake. Hiyo ni kweli. Unaona?

116 Kwa maneno mengine, unapaswa kuwa na cheche kwenye petroli, la sivyo hiyo petroli si zaidi ya . . . Hata haina thamani kama ya maji, mradi tu haina cheche ya kuiwasha moto. Kwa hiyo, hivyo ndivyo ilivyo.

117 Haidhuru tumefundishwa vizuri jinsi gani, tutaamini vizuri jinsi gani, na ni kiasi gani cha Biblia tunasema kwamba ni kweli, na tunaliamini lote kwamba ni kweli, haina budi kuwa ninii—dainamikia hazina budi kuwako, zile cheche, kuliwasha hilo Neno na kuifanya ianze kwenda. Haina budi kuwa na hiyo. Kama hufanyi hivyo, kanisa linakaa kimya, gari linakaa kimya, wewe utakaa kimya. Lakini haidhuru unasema, "Ninalifahamu jinsi gani. Ninaamini kila Neno Lake." Huna budi kuwa na kitu fulani cha kuliwasha hilo, kufanya hizo okteni mia moja zianze kuwaka, na Kanisa kubwa la Mungu lianze kupiga hatua.

Itabidi lichukue dainamikia pamoja na mitambo. Mitambo haina kasoro, bali inakosa dainamikia.

118 Nami ninafikiri hiyo ndiyo shida ya kanisa leo, tunakosa hiyo nguvu ya dainamikia, kulisukuma Neno hili na kulifanya liishi kwa ajili ya siku hizi.

119 Martin Luther alikuwa na mitambo na dainamikia, za siku yake. John Wesley alikuwa nazo, za siku yake. Pentekoste ilikuwa nazo, kwa siku yao.

120 Na siku yetu je? Huu ni wakati mwingine! Kanisa linapaswa kuwa limekomaa kabisa sasa, likiwa tayari kwenda kumlaki Kristo, pamoja na dhihirisho la kila baraka ambayo Yeye aliahidi katika Biblia, zikifanya kazi katika Mwili huo mmoja mkubwa ambamo Yeye aliahidi ya kwamba angekutana na watu na kuabudiwa, katika Kanisa Lake hili kuu.

121 Lakini, unaona, tunawapeleka watoto wetu shuleni, tunajifunza kusoma, kuandika, hesabu, historia yote ya manabii na kila kitu. Hilo ni sawa, lakini usipopata kitu fulani nyuma ya hiyo!

122 "Loo," unasema, "vema, ni—nilipaza sauti. Nilinena kwa lugha." Hayo ni mema. Ninaamini jambo hilo, pia. Bali hilo bado silo ninalonena habari zake. Unaona, uta—utaninii . . . litabwata. Unasema, "Plu-plu, boom-boom," kama gari la zamani likijaribu kwenda. Unasema, "Naam, ninaamini jambo *hili*. Ninaamini jambo *hilo*, pia. Lakini, lakini inapofikia kwenye *hili*, siku hizo, loo, la. La!"

123 Liko na okteni mia moja, ndugu, likiwa na jenereta sahihi nyuma yake, itahuisha kila Neno la Mungu litimize ahadi Yake. Hiyo ni kweli.

124 Hiyo ndiyo shida yetu leo, karibu tunafikia kikomo. Tunataka kuamini jambo *hili*, kuamini jambo *lile*.

125 Ninasema jambo fulani, juu ya Hili. "Vema, sijui." Vema, Biblia ilisema hivyo! Hilo linatosha. Kama Mungu alisema hivyo, liko hapo kutekelezwa. Kama sisi . . . Kama hilo ndilo Mungu alilosema lifanywe, yatupasa kulitekeleza hilo. Kaa hapo tu mpaka Mungu atakapohuisha, na ndipo moja kwa moja unaanza kukimbia basi tena, unaona. Usipofanya hivyo, plagi zote zitajaa moshi. Na kwa hiyo tunahitaji kitu fulani tofauti, tunataka kitu fulani cha kutuwasha moto.

126 Basi angalia, Yeye haingii tu kwa Roho Mtakatifu, kwa elimu ya Neno Lake, Yeye hulidhihirisha Neno hilo. Sasa kumbuka, manabii huliamini Neno. Hupokea Neno la Mungu. Ndipo Mungu Roho Mtakatifu aliingia ndani yao na kuiwasha moto ahadi hiyo, na kuifanya itimie. Loo, jamani! Ni nani atakayehukumu jambo hilo?

127 Yesu alisema, "Ni nani anayeweza kunihukumu kwamba nina dhambi? *Dhambi* ni 'kutokuamini.' Cho chote Mungu

alichoahidi na cho chote manabii walichosema, Mimi Ndimi Jibu lake. Yale waliyosema Mimi nitafanya, ninafanya." Yeye alikuja kama nabii, Mwana wa Adamu. Hivyo ndivyo alivyokuwa hasa, na ambalo alithibitisha kuwa. Alikuwa. Kwa nini? Dainamikia zilikuwapo pale zipate kuwasha moto mitambo. Yeye alikuwa ni mitambo, Mwana Mwenyewe, naye Baba alikuwa dainamikia. "Si Mimi ninayetenda kazi hizi, ni Baba Yangu anayeishi ndani Yangu. Yeye huchochea da—dainamikia na kufanya kitu hicho kiende. Anakitimiza."

128 "Ni wakati gani nilipata kusema jambo lo lote. . . " Kama vile Samweli alivyowaambia watu siku moja. "Je! nilipata kuwaambia jambo lo lote, katika Jina la Bwana, ila lile lililotimia?" Unaona? "Ni wakati gani nilipata kusema jambo hilo, na ni lini halikutimia?"

129 "Loo, wewe, yale uliyotwambia yalitimia, bali tunataka mfalme hata hivyo."

130 Hivyo ndivyo ilivyo siku hizi. Watu wanataka kushikilia mawazo yao yasiyo na maana. Wanataka kushikilia kanuni zao za imani. Wanataka kuzishikilia hizi. Wao wakinena habari za ufufuo katika siku zetu, tuanwezaje kuwa na ufufuo wakati mambo yote yamechafuka jinsi yalivyo? Petroli iliyotiwa maji na cho chote kile, kila namna ya sabuni na mambo haya yote ya kisasa yaliyochanganywa ndani yake.

131 Nilikuwa nikishuka kuja barabarani siku moja, na ikasemwa, namna fulani ya sabuni ya kisasa, ikasemwa, "Haikubidi kuosha vyombo, jambo pekee likupasalo kufanya ni kuvitumbukiza mle ndani kisha unavitoa."

132 Nikawazia, "Nitakuwa kijogoo nyumbani mwangu." Nitaenda nikajinunulie kopo la kitu hiki.

133 Ndipo nikamwambia mke wangu, "Nenda tu chumbani, mpenzi, acha nioshe vyombo."

134 Nikawazia, "Jamani, hao jamaa wanajua wanalozungumzia, hao wanasayansi. Nitamwonyesha mke jinsi mambo yalivyo. Nitaninii, yeye ataninii. . .mpaka atakapofahamu jambo hili, kile ninachofanya. Kutumbukiza tu na kuketi chini ukingojea, hivyo tu ndivyo inavyokubidi kufanya."

135 Watoto walikuwa wamekula mayai kwa kiamshakinywa. Ndipo nikamimina sabuni hii mle, na kuvitumbukiza, nikavitoa, nikazitumbukiza na kuzitoa. Zote zilikuwa zimejaa mayai. Naam, bwana. Siamini jambo lo lote ninalosikia kwenye televisheni, tena. La, bwana. La, la. La, katakata.

136 Hiyo ndiyo sababu siamini mfumo wo wote wa kujitengenezea unaweza kusimama. Mungu ana njia moja aliyoiandaa. Si Methodisti, Baptisti, Presbiteri, bali ni Yesu Kristo, kwa Kuzaliwa upya, kuiamini hiyo Biblia. Hiyo ndiyo njia ya Mungu aliyoiandaa, na njia pekee aliyo nayo, iko katika

Yesu Kristo, Mwanawe. Na, katika Mwanawe, Yeye aliliweka Jina Lake. Lake! Jina la Mungu ni Yesu, maana Yeye alikuja katika Jina la Baba Yake. Na kwa hiyo hilo lingekuwa ni Jina la Mungu, kwa maana Yeye alikuwa ni Mungu.

137 Sasa angalia, wakati nguvu hizi kuu za Mungu zinazotenda kazi zinapoingia katika mwana wa Mungu, humhuisha, Roho wa Uzima humwingia. Ndipo inafanya nini? Inawaweka katika ulimwengu wa Roho, sasa hivi. Si kwamba "watakuwa." Tuko sasa. Sasa tayari tumefufuliwa, dainamikia na mitambo zimeanza kutenda kazi, vimetuhuisha, nasi tumehuishwa tukapelekwa katika Uwepo wa Mungu, alipo Roho Wake. Na sasa tumeketi pamoja katika ulimwengu wa Roho, katika Kristo Yesu; katika Kristo Yesu, tukiwa tumeketi humo, kiti kile kikuu ambacho tayari kimewashwa moto, tumefufuliwa toka kwa wafu. Sisi ni sehemu ya hicho. Kama wewe ni sehemu ya Bibi-arusi, ndivyo ulivyo, kwa maana Bibi-arusi ni sehemu ya Bwana-arusi, mnajua. Kwa hiyo tunaona ya kwamba ni jambo lile lile. Naye atafanya vile vile hasa ilivyotabiriwa Kwake kufanya katika siku hii. Yeye hatakuwa Mlaodikia, hatakuwa vuguvugu kwa vyo vyote vile. Bali atakuwa moto kwa ajili ya Mungu, atakuwa akienenda katika Roho wa Mungu.

138 Sasa tunaangalia hapa sasa tupate kujua. Sasa hebu tuninii, sasa katika wakati uu huu linapofanya hivyo, ambapo hili linatugusa; na, wakati, tulikuwa wafu katika dhambi na kuasi, maasi, hasa, yeye. . . tumehuishwa pamoja katika Neno Lake la wakati huu.

139 Sasa hebu na tufikirie juu ya huko nyuma kabisa katika nyakati za kale, juu ya mtu fulani aliyehuishwa na Neno hili; kabla tu hatujafanya ibada ya kuwaombea wagonjwa. Hebu na tuchukue watu wachache, tuone tabia zao.

140 Hebu na tumchukue mtu hapa aliyetii Neno lote la Mungu, huko nyuma katika Agano la Kale, jina lake Henoko. Yeye alihuishwa sana na Neno la Mungu, hata alikuwa na ushuhuda, ya kwamba, "Alimpendeza Mungu." Hakuna jambo hata moja ambalo Mungu alimwagiza Henoko kufanya ila lile alilofanya.

141 Sijui ni akina Henoko wangapi wangekuwapo hapa alasiri ya leo, kwamba kama unajua liko katika Neno la Mungu? Ni wangapi wenu ninyi wanawake mliokata nywele zenu mngeweza kujiita wana Henoko, mnaona, mnaona, na mnajua ya kwamba Mungu analikataa jambo hilo? Ni wangapi wenu enyi wanaume, mnaowaruhusu wanawake wafanye jambo hilo, mngeweza kujiita Henoko? Loo, jamani! Hilo ni jambo moja tu, na yale maelfu je! Nasi tunalizima, tunasema, "Mimi ni mfuasi wa *hili*, nami ni mfuasi wa *lile*." Unaweza ukawa mfuasi wa hilo, lakini. . . mpaka utakapoingia katika mahali palipoandaliwa na Mungu! Wala huwezi kuingia mle isipokuwa ufanyike sehemu ya hilo Neno. Na, ukiwa ni sehemu Yake, unakuwa hilo lote,

na unalitii lote. Angalia, tuna kitu hiki hapa ambacho Biblia inakiita "Neno la Mungu," na, ambacho, ni Neno la Mungu.

142 Sasa tunaona ya kwamba Henoko aliingia katika njia iliyoandaliwa na Mungu, akiwa ana Neno Lake, na akatembea kwa muda wa miaka mia tano, na akampendeza Yeye. Nasi tunaona ya kwamba mitambo ilikuwa mikamilifu sana ndani Yake, hivi kwamba wakati dainamikia zilipoanza kutenda kazi katika injini, zilimwondoa tu duniani. Yeye alifanya safari ya kwanza ya kuruka kwa ndege, kitu kama hicho, kwenda Mbinguni. Akiendesha mitambo na dainamikia za Mungu, zote pamoja, "hakuonekana," kwa kuwa Mungu alimwondoa duniani, bila ya kuona mauti. Hiyo ni kweli kabisa. Alikuwa akitembea katika njia iliyoandaliwa na Mungu.

143 Ni jambo lile lile tunaloona kwa Eliya. Mzee Eliya alikuwa amewakaripia wengi sana wa hao Mayezebeli waliokuwa wamejipodoa nyuso, na mitindo ya kuktata nywele, na kadhalika, vitu walivyokuwa wakitumia siku hizo, mzee huyo alikuwa ameishi maisha yake akikemea tu dhambi miongoni mwa hao wanawake, kwa kuwa walikuwa na mwanamke fulani, Yezebeli, hapo wa kuwaongoza.

144 Ni kama tu Hollywood yenu hapa ilivyo nao, pia imewachukua dada wote ikawaviringishia katika jambo hilo huko. Na, huyo Yezebeli angali yu hai, unaweza tu kuangalia kila mahali na unaweza kuona ya kwamba angali hai. Na yungali katika mamlaka makuu, pia.

145 Sasa tunaona, mzee huyo akiwa ni nabii, alikuwa amekilaani kitu hicho na kila kitu, akadumu kikamilifu katika mapenzi ya Mungu. Wakati wahubiri wengine wote walipodhoofika, yeye alidumu pale pale pamoja Nalo.

146 Ndipo siku moja akawa amechoka sana, hata, Mungu akashusha gari la farasi chini kutoka Mbinguni, na farasi wa moto, na kumtwaa juu. Yeye alikuwa amejaa sana nguvu hizo za kuhuisha! Hebu wazia tu, akiwa na Neno la Mungu moyoni mwake, alijaa sana nguvu hizo za kuhuisha ambazo zilimhuisha!

147 "Ikiwa Roho wa Mungu, Yeye. . ." Ninaamini tunaona kwenye Warumi, 11, ama moja, 11. . . "Ikiwa," linasema, "Ikiwa Roho. . ." Warumi 8:11, ndipo lilipo. "Ikiwa Roho aliyemfufua Yesu katika wafu anakaa ndani yenu, ataihuisha pia na miili yenu ipatikanayo na mauti. Ikiwa Roho aliyemfufua Yesu katika wafu, ikiwa—ikiwa yumo ndani yenu, ataihuisha pia na miili yenu ipatikanayo na mauti."

148 Aliuhuisha! Maana ya neno *kuhuisha* ni nini? Neno hilo la Kiyunani linamaanisha "kufufuliwa baada ya kufa." Haleluya. Hilo hapo lango la kuabudia. Kuabudu katika Roho na Kweli, mitambo na dainamikia, pamoja. Unaona ninalomaanisha?

149 "Ikiwa Roho aliyemfufua Yesu katika wafu anakaa ndani yenu, ataihuisha, ataifanya hai, miili yenu ipatikanayo na mauti, kwa maana tayari ni Uzima." Na wakati unapoingia ndani ya mwili wako, inautiisha mwili wako wote Kwake. Kutii nini? Neno la Mungu. "Ikiwa yumo ndani yako."

150 Sasa kama ni kitu fulani kilicho ndani yako, kikikwambia, "Vema, hizo zilikuwa ni siku zilizopita. Na Marko 16 si kweli, na wazo hilo la Kipentekoste la ubatizo wa Roho Mtakatifu." Hiyo si Roho ya Mungu ndani yako. Sijali umefundishwa vizuri jinsi gani, wewe, hiyo si Roho ya Mungu. Unasema, "Vema, mama yangu alikuwa ni mfuasi wa *hili*, na baba yangu, kwa miaka mingi, na ndugu yangu." Lo lote unalotaka kusema juu ya jamaa yako, na kadhalika, huenda hilo lilikuwa ni sawa kwao; bali si sawa kwako, unaona, inakupasa kwenye siku hii uingie katika Kristo Yesu, kwa ajili ya wakati huu na ahadi iliyokusudiwa kwa ajili ya wakati huu.

151 Angalia, tunaona ya kwamba nguvu hii kuu ya kuhuisha ilimshukia Henoko, ikamhuisha na akaenda Nyumbani bila ya kufa.

152 Ilimwangukia Eliya, ikamhuisha hata akaenda Nyumbani bila ya kufa.

153 Tunaona ya kwamba mrithi wake alikuwa ni Elisha, ambaye ni mfano hapo wa Kristo na Kanisa, Elisha. Eliya alifanya miujiza minne, naye Elisha akafanya miujiza minane. Yeye alikuwa na sehemu maradufu, kama ile iliyomwagwa juu ya Kanisa. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] Baadaye walikuwa na maiti, wakaitupa juu ya mifupa yake, naye akafufuka. Hizo nguvu za kuhuisha zilikuwa kaburini pamoja naye. Huwezi . . .

154 Ziko hapo milele, unapopata nguvu hizo za kuhuisha za Mungu, ukihuishwa pamoja Naye sasa.

155 Sasa kumbukeni, katika Kristo, sisi ni mwili wa mwili Wake, mfupa wa mifupa Yake. Wakati Mungu alipomjeruhi Kristo pale Kalvari, Yeye alijeruhiwa kwa ajili yako na yangu. Sisi ni mwili wa mwili Wake, na mfupa wa mfupa Wake, mwili wa miwli Wake, Jina la Jina Lake, Bibi-arusi Wake. Unaona, sisi tumo ndani Yake, sisi ni mwili Wake na mifupa Yake.

156 Na Mungu ametufufua tayari, kwa siri. Zile nguvu za kuhuisha zilizotufufua kutoka katika maisha ya dhambi, na kubadilisha utu wetu, kwa uwezekano zimetufufua katika Kristo Yesu, ambapo, ufufuo utatufikisha katika utu uzima.

157 Sasa kumbukeni, sisi tulikufa katika jina letu wenyewe, tukazikwa, na kufufuliwa katika Lake. Unaona, sisi si mali yetu yetu wenyewe tena. Ambapo, Jina lile kuu la "Yesu Kristo" ambalo Biblia ilisema hapa katika Waefeso 1:21, ya kwamba, "Jamii zote mbili, Mbinguni na duniani, zinaitwa kwa Jina hilo." Hapo ndipo Mungu alipoweka Jina Lake. Hilo ndilo Jina la

familia iliyoko huko Mbinguni. Hilo ndilo Jina la familia hapa duniani.

158 Nasi tuko ndani ya Yesu Kristo, kwa ubatizo wa kiroho, si kwa maji; kwa Roho, tumebatizwa katika Mwili mmoja, ambao ni Kristo, mahali pa kuabudia. Basi, tukiwa mle, tunakuwa kwenye shamba hili, ni kama hatimiliki dhahania.

159 Unasema, "Nilinunua shamba fulani." Si yako bado mpaka utakapopata dhahania. Lakini kama una dhahania, inaonyesha ya kwamba kila kitu kilichowahi kupinga shamba hilo kimefutiliwa mbali.

160 Na ndipo wakati umekwisha kuwa Mkristo na kumkubali Kristo kama Mwokozi wako, basi, wakati Mungu anapoishusha dhahania, inaonyesha ya kwamba haidhuru baba yako alifanya nini, mama yako alifanya nini, kile mtu ye yote alichofanya; mama yako, baba yako huenda walikuwa ni walevi, malaya; cho chote kile, kila dhambi imefutiliwa mbali! Una hatimiliki dhahania. Hakuna kitu kinachoweza kukuondoa kwake. Tena, angalia, kila kitu kilichoko kwenye hilo shamba ni chako! Amina. Na wakati unapokuwa katika Kristo Yesu, kwa ubatizo wa Roho Mtakatifu, kila karama ya Mungu ni mali ya Kanisa. Amina. Ni hatimiliki dhahania. Wewe, ni yako, ni mali yako. Inaihuisha miili yenu inayopatikana na mauti. Loo, jamani, laiti tungaliwazia jambo hilo!

161 Hebu tuwaangalie wale waaminifu hapo Pentekoste. Wote walikuwa katika chumba cha juu kule, na wote walikuwa wana hofu. Walikuwa na, walikuwa na ninii—hatimiliki, ndio, bali walikuwa wanahofu. "Mara kukaja toka Mbinguni uvumi," ile dhahania waliyotumiwa, "kama uvumi wa upepo wa nguvu ukienda kasi, ukaijaza nyumba yote waliyokuwa wameketi." Nao walihuishwa sana na Hiyo, mpaka uwoga wao wote uka-. . . Mmoja wao hata alikuwa anahofu, wao hata walikana kwamba yeye hakuwa Mfarisayo bado, ama hakuwa Msadukayo bado. Lakini wakati Roho Mtakatifu huyo aliposhuka na kumbatiza katika Yesu Kristo, yeye alifanyika mwili wa Mwili Wake, mfupa wa mfupa Wake, Neno la Neno Lake. Alikuwa ni kiumbe kipya. Alikuwa ni mtu mpya. Ilihuisha mwili wake.

162 Angalia kile ilichofanya, kile inachofanya wakati inapoingia ndani. Haikufanyi utoke nje na kusema, "Mimi ni Mmethodisti. Mimi ni Mbaptisti. Loo, ninajua sipaswi kuvuta sigara. Sipaswi kuwa na *hili*. Sipaswi kuvaa nguo za aina *hii*. Sipaswi kufanya jambo *hili*. Sipaswi kufanya jambo *lile*." Inakuhuisha sana mpaka inakulazimu kufanya jambo hilo. Inaihuishi miili yenu ipatikanayo na mauti.

163 Angalia, ilihuisha miili yao ipatikanayo na mauti, mpaka wakaruka karibu sana na Mbinguni mpaka ikauhuisha mwili wao kunena katika lugha ambayo hawajawahi kusikia hapo awali. Iliihuisha miili yao, wakanena katika lugha mpya ya

Mbinguni. Walihuishwa wakaingia katika Uwepo wa Mungu, kwa ubatizo wa Roho Mtakatifu. Nguvu za kuhuisha za Mungu ziliwabatiza wakaingia humo. Ndipo wakawa katika mahali pa kuabudia basi. Walikuwa mahali ambapo wangeweza kuabudu. Lile Baraza la wazee wala cho chote kile visingeweza kuwasumbua, kwa maana walikuwa wamehuishwa. Walikuwa ni watu wapya. Hiyo ni baada ya wao kubatizwa.

164 Hebu mwangalie maskini Stefano. Yeye aliingia kwenye njia iliyoandaliwa na Mungu, akahuishwa na nguvu za Mungu; akaingia kwenye lango, njia iliyoandaliwa na Mungu. Na hata wakati walipoenda kumwua, kumpiga mawe hata afe, yeye alisema, "Naona Mbingu zimefunguka, Yesu amesimama mkono wa kuume wa Mungu." Hizo ni nguvu za kuhuisha. Yeye alihuishwa akaingia kifuani Mwake.

165 Kulikuwa na Filipo, mwingine aliyekuwa amejaa nguvu za kuhuisha. Tunamwona kule sehemu za Samaria, akifanya mkutano mkubwa wa ufufuo. Nguvu hizi kuu za kuhuisha, baada ya yeye kuwa ndani ya Kristo, zilishuka zikaja mahali ambapo alikuwa akisikilizwa na maelfu ya watu. Ndipo akasema, "Sasa ondoka hapa, Filipo, ninataka utoke uende kwenye nyika hii, Gaza, hapa. Nina mtu fulani kule, ninataka ukakutane naye." Wala hakuna swali, hakuna swali hata kidogo, yeye alikuwa amejaa hizo nguvu za kuhuisha. Alikuwa katika Kristo, alikuwa mahali palipoandaliwa ambapo Mungu aliweza kusema naye. Mungu alisema naye. Hakukuwako na swali.

166 Unasema, "Vema, Yeye alisema nami na kuniambia nitaponywa, lakini, sasa, sijui, ninajisikia vibaya sana leo." Loo, jamani! "Vema, Yeye aliniambia nilikuwa nina Roho Mtakatifu, na wakati mwingine hakika ninashuku jambo hilo."

167 Filipo alijua Sauti ya Mungu barabara, maana yeye alikuwa amekuja kwa njia iliyoandaliwa na Mungu. Hakumuuliza Mungu swali, juu ya, "Vema, Mungu, nina wengi sana hapa, sina budi kusimama. Inanibidi nimwone mzee wa jimbo kabla sijafanya jambo hilo. Inabidi niende nikazungumze na askofu," hapakuwa na kitu kama hicho. Yeye alimjali Mungu, moja kwa moja nyikani akaenda!

168 Akamwona mtu mmoja, towashi, Mkushi, mtu mweusi akishuka akija, akisoma Maandiko katika Isaya. Ndipo akasema, "Je, unaelewa na hayo unayosoma?"

Akasema, "Nitawezaje mtu asiponifundisha?"

169 Filipo akaingia kwenye lile gari na akaanza kuzungumza naye habari za Bwana.

170 Akasema, "Maji haya, ni nini kinachonizuia nisibatizwe?"

171 Akasema, "Kama ukiamini kwa moyo wako wote, nafsi yako yote na akili zako zote, na nguvu." Akashuka kwenye lile gari akambatiza.

172 Naye Filipo alikuwa amejaa sana hizo nguvu za kuhuisha, hata, Yeye alimtwaa asimwone tena. Wazia! Katika mwili wake unaopatikana na mauti, mwili wake wa nyama ulitwaliwa, asionekane machoni pa huyo towashi. Ninaamini hilo kuwa ni kweli. Mungu angeweza kumpeleka mahali pengine, ambako alikuwa ana haja naye. Alitwaliwa juu.

173 Unajua, mauti hata hayawezi kukiondoa kitu hicho kutoka kwako, unapokuwa katika Kristo, katika mahali alipo Mungu.

174 Angalia hapa, Musa alikuwa nayo. Alikuwa ni nabii ambaye alijiliwa na Neno la Mungu. Hakuna wengi . . . ni Kora wangapi walioinuka na kusema, "Tunahitaji madhehebu makubwa. Sasa wewe unajaribu kuchukua mahali pa kuwa mtu pekee aliye mtakatifu." Mungu akasema, "Jitenge, nitammeza tu." Na akina Dathani, na kadhalika, hakuwajali, alisonga mbele moja kwa moja.

175 Na wakati Musa alipokufa na akazikwa, na wale Malaika, zile nguvu za kuhuisha zilikaa pamoja naye. Kwa kuwa, miaka mia nane baadaye, huyu hapa huko kwenye nchi ya ahadi, akizungumza na Yesu. Hizo nguvu za kuhuisha zilikuwa zingali juu yake. Hapo ndipo mahali pa Mungu pa kuabudia.

176 "Ati nini? Ulijuaje?" Yeye alikuwa ni nabii. Neno lilimjia nabii. Naye alikuwa Neno la Mungu lililodhihirishwa kwa wakati wake. Amina.

177 Unaona, huwezi kufa, umekwisha kuhuishwa. Loo, laiti kanisa lingaliweza tu kuona jambo hilo, ya kwamba si kile unachoenda kuwa, uko hivyo tayari! Ni Ibilisi anayejaribu kukunyang'anya kitu hicho.

178 "Vema," unasema, "sasa nitakwambia. Mimi ni mfuasi wa *hili*." Sijali wewe ni mfuasi wa kitu gani.

179 Inakupasa kuzaliwa mara ya pili, kuzaliwa upya, ubatizwe na Roho Mtakatifu, ndani ya Yesu Kristo, uhuishwe kwa kila Neno. Roho yako, ndani yako, itaitikia "amina" kwa kila Neno la Biblia. Nje ya jambo hilo, kama hiyo—kama ikitikisa kichwa chake juu ya jambo moja, tupilia mbali roho hiyo. Si Roho ya Mungu ambayo ingeshindana na Neno la Mungu. Itadumu na Neno la Mungu. Si kwamba tu inaliamini, bali inalifanya kuwa hai. Inadhihirisha Neno la Mungu. Naam, bwana.

180 Waangalie pia hao watakatifu wa Agano la Kale. Kwa uwezekano, chini ya ile dhabihu ya kale, wao walikuwa wakingojea hii mpya ije, walikuwa na dhamiri njema kwa Mungu. Katika mathayo 27, tunaambiwa jambo hilo, wakati Yesu alipofufuka na akatoka kaburini. Ambalo, ndiyo kwanza tusherehekee hilo majuma machache yaliyopita, Pasaka. Biblia ilisema ya kwamba, "Wengi wa hao watakatifu waliokuwa wamelala katika mavumbi ya nchi, walifufuka kwenye kufufuka Kwake, wakaingia mjini na kuwatokea wengi." Walikuwa ni kitu

gani? Walikuwa ni madhihirisho ya Neno la Mungu lililoahidiwa. Mahali pekee ambapo Mungu anakutana, chini ya ile dhabihu.

181 Sasa katika Wathesalonike wa Kwanza 4:16, Biblia ilisema, pia, ya kwamba watakatifu wa Agano Jipya wangejitokeza pamoja Naye atakapokuja tena, hao waliohuishwa ndani Yake sasa. Unaingiaje ndani Yake? Kwa ubatizo wa kiroho, nguvu za Mungu, mahali ambapo Yeye anakutana, katika Yesu. Sasa Yesu ndiye njia iliyoandaliwa na Mungu.

182 Sasa angalia, Yesu alikuwa na hakika mno kile alichokuwa! Yeye alijua alikuwa ni Mwana wa Mungu. Alijua alizaliwa na bikira. Alijua ya kwamba kila Andiko lilidhihirika moja kwa moja kupitia Kwake. Alijua jambo hilo kikamilifu kabisa, hata akawaambia hao wajenzi wa hekalu, siku ile, Alisema, "Liharibuni, nami nitalifufua katika siku tatu." Wazia jambo hilo. "Liharibuni, Nami nitalifufua katika siku tatu." Kwa nini? Lilikuwa ni Neno lililoandikwa juu Yake.

183 Daudi alisema, "Sitamwacha Mtakatifu Wangu kuzimu, sitaiacha nafsi Yake katika kuzimu, wala sitamwacha Mtakatifu Wangu aone uharibifu."

184 Sasa, Yesu alijua ya kwamba huyo alikuwa ni Yeye. Hakuwa na swali moyoni Mwake. Naye alijua ya kwamba, masaa sabini na mawili, mwili huoza, wakati fulani katika masaa hayo sabini na mawili Yeye atakuwa hai tena, kwa hiyo akasema, "Liharibuni hekalu hili, Nitalifufua tena katika siku ya tatu." Kwa nini? Neno hilo liliandikwa juu Yake. Liliandikwa juu Yake, kwa maana yeye alikuwa ni dhihirisho la Neno la Mungu lililoandikwa kwa ajili ya siku ile.

185 Vema, inabidi kuwe, haleluya, inabidi kuwe, ndugu, pale mahali fulani, Neno la Mungu lililodhihirishwa la siku ya leo. Na hilo ni jambo lile lile, kwa maana Yeye alinena habari za siku hizi Naye akasema ni jambo gani lingetukia katika siku hizi. Amekwisha tuambia. Tunajua kitakachotukia. Nasi tukiona kikidhihirishwa ndani yako, basi wewe umo katika Kanisa la Mungu. Nje ya hilo, ungeweza kujiita "Mmethodisti, Mbaptisti," ama kitu cho chote kile, haitafaa kitu. Kulikuwako na mahali pamoja tu pa kukutania, hapo ni katika Kristo Yesu. Loo, leo, loo, laiti siku hizi kila mtu angaliona jambo hilo, aone jinsi ya kuingia, akibatizwa. Bibi-arusi ni sehemu ya Mumewe. Kanisa ni sehemu ya Neno, lile dhihirisho.

186 Sasa wewe umo katika kanisa lipi? Je! umo katika madhehebu? Kama ndivyo ulivyo, nitakwambia waziwazi sana sasa, wewe umo katika Laodikia. Lakini kama wewe uko ndani ya Kristo, wewe ni kiumbe kipya, nawe uko ndani ya Kanisa la Mungu aliye hai, ukiwa na dhihirisho la mambo yale yale aliyofanya katika siku Zake litakuwa likirudi hapa katika siku hizi, ukifanya jambo lile lile alilosema ya kwamba lingefanya. Ndipo, hilo ndilo Kanisa halisi. Unaingia ndani Yake kwa

ubatizo wa kiroho, si kwa kujiunga, si kwa mambo mengine, bali kwa kubatizwa na Roho Mtakatifu kuingizwa katika Mwili Wake. Sawa. Ni njia pekee iliyoandaliwa na Mungu ambayo ametuachia kufanya, ni kubatizwa katika Mwili Wake, kwa Roho Wake.

187 Yesu alisema, katika Yohana Mtataktifu 14:12, "Yeye aaminiye, akiwa ndani Yangu!" Si ajabu watu husema ya kwamba siku za miujiza zimepita, si ajabu wanasema mambo haya. "Yeye aniaminiye Mimi, si mwenye mwelekeo wa kuniamini Mimi, bali aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi, yeye naye atazifanya." Kwa nini? Ni Uzima Wake. Ni dainamikia zake katika mitambo Yake, zilizo ndani yako, zinazoliwasha moto hilo, zinalifanya liende na kufanya kazi ilizoahidiwa kufanya. Ama, uhai wangu ndani Yake, umenihuisha kwa Roho Wake, kulifanya Neno Lake, ambalo ni mitambo, kutenda kazi kwa dainamikia Zake. Waebrania 13:8, "Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele."

188 Sasa pia katika Marko mlango wa 17, kifungu cha 30, cha Marko Mtakatifu. Sikilizeni kwa makini. Yesu aliahidi mambo haya katika siku za mwisho, ya kwamba Yeye ni "yeye yule jana na hata milele." Aliahidi, katika Malaki 4, ya kwamba "angeigeuza mioyo ya watu, katika siku za mwisho, iirudie Imani ya baba zao." Aliahidi jambo hilo. Aliahidi, mahali pengi sana katika Biblia, mambo ambayo angefanya. "Bado kitambo kidogo na ulimwengu hautaniona tena, bali ninyi mtaniona; nitakuwa pamoja nanyi, ndani yenu daima, hata ukamilifu wa dahari." Pia angalia katika Luka Mtakatifu tena, 17:30, "Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma!"

189 Mnajua jambo lililotukia huko Sodoma? Angalia huko California; si California peke yake, Marekani; si katika Marekani peke yake, bali ulimwenguni.

190 Angalia kichaa hiki cha matineja! Mbona, tulikuwa na . . . Niliwaambia hivi majuzi, walikuwa wakifanya utafiti kule wa shule za Arizona ambako mimi ninaishi, na asilimia themanini ya watoto shuleni wamevia akili. Je! watoto wao watakuwa kitu gani? Hatuwezi kuwa na kizazi kingine. Tuko mwisho. Yesu alisema mambo haya yangekuja.

191 Angalia televisheni zote na kadhalika vikiandaa vitu hivi vya uongo. Wakati unakuja, ninabashiri, ambapo watu watakuwa vichaa barabara, kabisa, Ulimwengu utakuwa kichaa. Biblia inazungumza juu ya vitu vya kutisha sana kama vile wanavyoonyesha katika sinema siku hizi, za baadhi ya mayai ya viumbe vilivyokuwapo kabla ya kuandikwa kwa historia, vilivyoishi duniani miaka elfu nyingi sana na mamilioni ya miaka, vinazaa na kujitokeza kwenye ninii. Hicho ni kitu kidogo tu, ukilinganisha na yale yatakayotukia. Wakati kuzimu kutakapofunguliwa na Ibilisi atoke pamoja na vitu vyake vyote

vya ajabu, kuhusu wanawake. . . ama nzige wenye nywele kama za wanawake, na meno kama ya simba. Mbona, ulimwengu utakuwa kichaa barabara, kabisa. Imefikia tu hatua moja hivi kutoka kwenye uendawazimu sasa.

192 Loo, laiti ningaliuhisi utukufu wa Mungu, kule Kuja kwa Bwana Yesu, Roho Mtakatifu, kulijua hilo, ule Uwepo ulio hai wa Mungu aliye hai!

193 Yesu alisema, katika Marko Mtakatifu pale, alisema, "Katika siku hiyo Mwana wa Adamu atafunuliwa." Sasa, kumbukeni, si Mwana wa Mungu. Yeye alikuja katika majina matatu ya wana: Mwana wa Adamu, Mwana wa Mungu, Mwana wa Daudi. Wakati Yeye alipokuwa hapa duniani, alikuja kama Mwana wa Adamu, Yeye alikuwa ni nabii. Mwana wa Adamu ni nabii. Yehova Mwenyewe aliwaita manabii, Yeremia na hao wengine, "Mwanadamu, unaona kitu gani?" Yesu alikuja, kwa kuwa ilibidi aje kulingana na Maandiko, kama Mwana wa Adamu. Musa alisema, "Bwana Mungu wako atawaondokeshea Nabii, kwa mithili yangu." Naye ilibidi awe ni nabii, Mwana wa Adamu.

194 Lakini baada ya mauti Yake, kuzikwa, na kufufuka, Yeye sasa amekuwa ni Mwana wa Mungu, wa kimbinguni, Roho Mtakatifu.

195 Lakini aliahidi, kabla tu ya kuja kwa wakati wa mwisho, ulimwengu utakuwa kama ulivyokuwa katika Sodoma, wakati Mtu fulani aliposhuka katika umbo la mwanadamu; watu watatu, Malaika wawili pamoja na Mungu Mwenyewe. Huyo alikuwa ni Mungu. Biblia ilisema alikuwa ni Mungu. Sasa Yeye alishuka na kujidhihirisha Mwenyewe pale, kwa kugeuza mgongo wake kuelekea he—hemani ambako Sara alikuwa, naye akamwambia Ibrahimu yale Sara aliyokuwa akiwazia hemani. Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Sasa, Yesu Mwenyewe alisema, "Katika siku atakapofunuliwa Mwana wa Adamu," kwa maneno mengine, "Mwana wa Adamu, ile huduma ya Yesu Kristo Mwenyewe."

196 Kanisa litapitia katika kuhesabiwa haki, kupitia kwa Luther; litapitia katika utakaso, kupitia kwa Wesley; litapitia kwenye ubatizo wa Roho Mtakatifu, na Wapentekoste; na kuingia moja kwa moja katika ukamilifu wa Mwana wa Adamu, wakati ambapo Mume na Mke watakapokuwa ni wamoja. Mungu atadhihirishwa sana katika Bibi-arusi Wake, Kanisa Lake, mpaka wote wawili watakuwa wamefanana. Wao ni mmoja. Sasa mnaona mahali tulipo.

197 Msishikilie hayo mapokeo na kanuni za imani. Hayo yalikuwa ni sawa katika zama zao, bali ua limesitawi likachanua sasa. Ni wakati wa mbegu. Hiyo ni kweli.

198 Yesu aliahidi mambo haya. Sasa wakati tunapomwona Mungu akifanya ahadi Yake kuwa hai mbele zetu, na kuona

ya kwamba imo ndani yetu, na Roho Wake anaishi ndani yetu; hiyo ndiyo njia pekee ya kuabudu, mahali pekee pa kuabudia, njia pekee ya kweli unayoweza kuabudia, "Kwa maana hakuna hukumu ya adhabu kwa hao walio katika Kristo Yesu." Mungu alitoa ahadi. Yesu alisema, "Mambo haya nifanyayo, nanyi pia mtayafanya," na yale Yeye angefanya katika siku ya mwisho. Jinsi lilivyopitia katika wakati huu, si nuru wala mchana, ingekuwa ninii—kama wakati wa giza, lakini alisema, "Wakati wa jioni, itakuwa Nuru."

199 Jua linachomoza mashariki na kutua magharibi. Jua lile lile linalochomoza mashariki hutua magharibi, ustaarabu umesafiri pamoja nalo. Umesafiri juu ya mafungu matatu ya maji, aina tatu za ubatizo. Loo, ndio, kutoka Asia, ukavuka ukaingia Ulaya; kutoka Ulaya, ukaingia Uingereza; na kutoka Uingereza, ukaingia Marekani.

200 Na sasa tumerudi moja kwa moja tena, na hapa tumeketi alasiri ya leo, kwenye Pwani ya Magharibi, ambako tuta la dhambi za nguvu zote za giza hurundikana humu. Hawa wachezaji wa sinema na televisheni, na wanaume wakiwabusu wanawake humo, na kutia sumu akili za wasichana wadogo.

201 Je! ulijua mwanamume ye yote anayembusu mwanamke anawajibika kimaadili kumwoa? Kwa uwezekano ni tendo la kujuana kimwili. Hakika, ndivyo ilivyo. Ndio, bwana. Ni kitu gani? Ni hizo tezi za kiume katika mdomo wa mwanamume, na tezi za kike. Wakati tezi za kiume na za kike zinapokutana, ni kujuana kimwili.

202 Angalia huko Hollywood, angalia hao wasichana wadogo wanaolala hapa nje kwenye bustani, na vijana wakigaagaa juu ya wasichana hawa, na mambo kama hayo, na hata wanaimba kwenye kwaya. Na hawa akina Elvis Presley, na kadhalika, tulio nao siku hizi, ni fedheha kwa jina la Marekani, kwa yale babu zetu waliyopigania na kumwaga damu na kufia.

203 Bali wakati umewadia ambapo kila taifa halina budi kuanguka, kwa kuwa kuna Ufalme wa Mungu ulioanzishwa katika moyo wa mwanadamu, kwa ubatizo wa Roho Mtakatifu na Uwepo wa Yesu Kristo. Na Kristo atakuja kwa Bibi-arusi Wake na ataanzisha Ufalme hapa duniani, ambao hautaondoshwa kamwe. Unaingiaje katika Ufalme huu? Unazaliwa ndani yake. Unajuaje jambo hilo? Unaendelea tu . . . Ungewezaje kuwa raia wa ufalme fulani na kubishana na mfalme wake? Unaona, ungeninii . . . Naye huyo Mfalme ni Neno. "Hapo mwanzo kulikuwako Neno, Naye Neno alikuwako kwa Mungu, Naye Neno alikuwa Mungu. Naye Neno alifanyika mwili na akakaa kwetu. Yeye yule jana, leo, na hata milele."

204 Wao walijuaje Yeye alikuwa ni Mwana wa Adamu? Yeye angeangalia huko kwa wasikilizaji na kujua yale waliyokuwa

wakiwazia. Tunajua jambo hilo ni kweli. Ni yeye yule leo. Je! mnaamini jambo hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

205 Je! Billy alisamabaza kadi zo zote za maombi? Hilo ndilo nilisahau kumwuliza. Je! alisambaza kadi za maombi? [Kusanyiko linasema, "Ndio."—Mh.] Je! alisambaza kadi za maombi? Sawa.

206 Nitawaambia. Kama mna imani ya kutosha, mimi nina imani ya kuamini ya kwamba Mungu, Yeye aliyetoa ahadi, anaweza kujithbitisha kwamba Yeye ni Mungu papa hapa, bila ya mtu ye yote kuja kwenye jukwaa hili. Ninajisikia kuchukua hatua ya kwanza, kwa sababu ya ahadi ya Neno la Mungu aliye hai. Angalieni hapa, hebu niwaonyeshe jambo fulani. Hii nguvu ya kuhuisha, tutaifanyia zoezi. Hebu niwaonyeshe. Ni wangapi wanaoamini ya kwamba mna nguvu hizo za kuhuisha? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Vema, hivi mikono yenu ina nini ikiwekwa juu ya wagonjwa?

207 Wakati hao wanafunzi walipopokea nguvu za kuhuisha juu yao, kwenye Siku ya Pentekoste, wao walifanya kitu gani? Walitoka wakaenda wakaweka mikono yao juu ya wagonjwa, nao wakapona. Yesu alisema, katika Marko 16, "Itaendelea mpaka utimilifu wa dahari." Muda gani, mpaka kwenye wakati wa mitume? "Enendeni ulimwenguni kote, mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe. Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio; wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya." Hizo ni nguvu za kuhuisha kama zilizokuwa juu ya mifupa ya Eliya, mifupa ya Elisha. Na nguvu zile zile za kuhuisha ziko juu ya watakatifu ambazo zimewafufua. Kama nguvu zizo hizo za kuhuisha zimo ndani yetu, wekeni mikono yenu juu ya wagonjwa, watapona.

208 Nimeona hapa, karibu niache kupambanua, tena, ninaweka tu mikono yangu juu ya wagonjwa. Nimekuwa nikiona wakati, jamani, mambo ambayo kamwe sijaninii . . . Sikufikia theluthi moja ya watu, hata hivyo. Kwa njia hii, ninawafikia wengi zaidi kuliko nilivyowahi kufikia. Nami ninapata matokeo mazuri zaidi, kwa kujiweka tu katika mikono ya Mungu, na kusema, "Bwana Mungu, Wewe uliahidi jambo hilo. Ni ahadi Yako; si yangu mimi, ni Yako, Nawe uliahidi utaitimiza. Nami nimekuona ukifanya jambo hilo. Nami nitaamini ya kwamba utafanya hivyo, kwa kuwa nimebatizwa katika Mwili Wako, na Roho Yako hapa kutambulisha ya kwamba hilo ni Kweli." Amina. Hapo ndipo mahali pa kuabudia. Ndipo unafikia mahali, "mambo yote yanawezekana." Ndipo unafikia mahali ambapo ninii yako—ambapo nia na kusudi lako, kwa maana mafanikio yako, yako hasa katika mapenzi ya Mungu. Na wakati unapoweka mikono yako pale na kuamini, litatukia. Je! mnaamini jambo hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

209 Ninaamini, kabla hata kadi moja haijaitwa, ama jambo lingine lo lote, ya kwamba Mungu Mwenyezi anaweza kuniambia

ulicho nacho huko, na kile unachopaswa kuwa umefanya, na yale usiyopaswa kufanya. Huko ni kuanza kufanya jambo, naam, ninajua hiyo ni kweli, bali hilo ni jambo lile haswa ambalo Mungu angetaka tufanye. Je! mnaamini jambo hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Je! ni wangapi mngeamini jambo hilo kama Mungu angelilifanya? ["Amina!"]

210 Hakuna mtu anayeketi mbele zangu ninayemjua, ambaye ninaweza kumwazia, ama kuona mtu ye yote ambaye kwa kweli ninamjua kweli. Ni wangapi wanaojua, hapa, sisi hatufahamiani, inueni mikono yenu. Wanaojua kwamba siwajui kabisa, inueni mikono yenu. Po pote katika wasikilizaji, anayejua sikujui kabisa. Nadhani ni kila mahali, hasa upande huu. Sasa huenda hao watu wengine waninii tu. . . Siwajui. Hawakuinua mikono yao tu, lakini si—si—siwajui, hata hivyo. Ninaamini ninamwona Richard Blair ameketi papa hapa. Ninaamini hiyo ni kweli. Ninaweza. . . Kuna giza huko chini. Kuna nuru upande *huu*. Sioni.

211 Lakini angalia hapa, ninajaribu kuwaambia, ya kwamba, wakati hizo nguvu za kuhuisha zinapokuja ndani yako, ni Yesu Kristo. Yesu alipoweka mikono Yake juu ya wagonjwa, walipona.

212 Wakati Yesu alipokuwa na nguvu za kuhuisha kumhuisha, kama Mwanadamu, Yeye angeweza kuangalia huko nje na kujua mawazo yaliyokuwa juu ya watu, kuwaambia waliyokuwa wakiwazia, yale waliyofanya. Anawapa kisogo, anawaambia jambo lile lile, "Kwa nini mnahoji mioyoni mwenu?" Yule mwanamke aligusa vazi Lake, Yeye akasema, "Ni nani aliyenigusa?" Akaangalia kote akampata, na kusema, "Ninaona nguvu zimenitoka. Imani yako imekuponya." Huyo ni Yesu Kristo. Hiyo inathibitisha hapo ndipo kanisa lilipo, na vile nguvu halisi za kuhuisha za Mungu zinavyomfanyia mwanadamu. Je! mnaamini jambo hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

Hebu na tuinamishe vichwa vyetu kwa muda mfupi tu.

213 Mungu mpendwa, tulikuwa na vita na Shetani alasiri ya leo, kwenye maikrofoni hizi, tukijua hao watu labda hawakusikia nusu yake, huko kurudishwa kwa mwangwi kwenye. . . katika jengo jinsi hiyo. Bali ninaomba, Mungu, ya kwamba Roho Mtakatifu atachukua kile kilichokusudiwa kuwa, Bwana, kuwaacha watu waone ya kwamba sisi si kundi fulani lililokufa linalojikokota na linalotumainia mambo fulani fulani. Mungu, sisi tuko hai sasa, tumehuishwa na nguvu za kufufuka Kwake Kristo. Yesu Kristo anaishi ndani yetu. Tunaamini jambo hilo, Bwana.

214 Hatudai utukufu wetu wenyewe. Kama vile kwenye Mlima wa Kugeuzwa, ambapo kila mmoja wetu amewakilishwa pale; kulikuwako na Musa, yule aliyekufa na kufufuka tena; kulikuwako na Eliya, wale watakatifu wa kuhuishwa ambao

watatwaliwa juu katika siku ya mwisho. Loo, waliona basi, walipoangalia nyuma, walimwona Yesu pekee. Tunajua, Bwana, hatutaki watu watuone sisi. Hatuko hapa kwa kusudi hilo. Sivyo kabisa!

215 Lakini, Bwana, inafurahisha mioyo yetu tunapomwona Yesu ametukuzwa miongoni mwetu; tunapomwona ametukuzwa, tunapolioana Neno Lake, ambapo Yeye ni Neno; wakati tunapoona kwamba tunaweza kulisoma hapa katika Biblia, ambapo Yeye aliahidi angefanya jambo hilo, halafu tunamwona akilitekeleza moja kwa moja ndani yetu, Ee Mungu, jinsi inavyotufanya tujisikie wanyenyekevu, kwamba tunajua ya kwamba Uwepo Wake ulio hai . . .

216 Hatujajiunga na kitu cho chote wala kupigania kitu cho chote. Tunaamini tu, Bwana, hadi Uzima wa Milele. Nawe ulitutia muhuri mle ndani kwa ubatizo wa Roho Mtakatifu, kisha ukaihuisha miili yetu, na kuzihuisha roho zetu, na kutuhuisha sisi basi tupate kuona maono, na kutabiri, na kunena kwa lugha, kuona ishara kuu na maajabu yakitendeka. Mbona, ni Mungu aliye hai. Sisi tumo katika huo Mwili. Wakati, kwa ulimwengu, ni upumbavu kwa hao waangamiao; bali kwetu sisi tunaoamini, ni nguvu za Mungu, hadi Uzima wa Milele. Tunakushukuru kwa ajili ya jambo hilo, Baba.

217 Sasa na ijulikane siku ya leo, Bwana, ya kwamba Wewe ni Mungu, ya kwamba hujabadili nia Yako juu ya Neno moja ulilopata kusema. Na ni Wewe yeye yule jana, leo, na hata milele, na Njia ile moja—moja na ya pekee ambayo Mungu ameiandaa. Mtu pekee ambaye Mungu aliwahi kuweka Jina Lake ndani Yake, alikuwa ni Mwanawe Mwenyewe Ambaye alibeba Jina Lake, Yesu; Mungu, Yehova, Mwokozi, Imanueli, Mlango wa zizi la kondoo; Yeye Aliyekuwako, Aliyeko, na Atakayekuja; Shina na Mzao, Shina na Mzao wa Daudi pia; Nyota ya Asubuhi, Ninyoro ya Bondeni. Ee Mungu, jinsi lilivyo la ajabu! Si ajabu Isaya alisema, "Mshauri, Mfalme wa Amani, Mungu Mwenye Nguvu, Baba wa Milele." Loo, hatuna Baba mwingine ila Wewe, Bwana. Wewe ndiwe Baba yetu. Wewe ndiwe Mama yetu. Wewe ni yote tuliyo sisi, yote ambayo tungeweza kuwa. Hatutaona kitu kingine cho chote ila Yesu aliyetukuzwa!

218 Baba, huenda sikuuhubiri huu vizuri, alasiri ya leo, bali chukua nia ya moyo wangu, na unisikie; Mungu mpenzi. Na jalia isemwe, leo, ya kwamba Yesu Kristo alitukuzwa papa hapa katika hekalu hili. Tujalie, Baba, kwa kuwa tunaomba katika Jina Lake, na ninapongojea kwa unyenyekevu pamoja na wasikilizaji hawa, kukuona ukitenda kazi kwa Roho Yako. Amina.

219 Sasa ninawatakeni mnifanyie jambo hili moja. Ninataka kuwaulizeni swali moja zito. Ninawatakeni mnijibu kana kwamba ilikuwa ndiyo mara ya mwisho ambayo mngeweza

kumjibu mtu ye yote maishani mwenu. Je! mnaamini jambo hilo ni Kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Je! Mnaamini hakuna kanisa wala madhehebu yangeweza kutambuliwa katika Uwepo wa Mungu? Mnaamini jambo hilo? ["Amina."—Mh.] Hakuna hata moja. Ni wale tu waliozaliwa katika Yesu Kristo, wanaochukua Jina Lake! Hiyo ni kweli.

220 Unachukua Jina Lake wakati unapozaliwa mara ya pili humo ndani, si kwa ubatizo wa maji. Ingawa unaweza kubatizwa katika Jina Lake, lakini huo haulichukui Jina Lake. Unalichukua Jina Lake kwa kuzaliwa, si kwa maji. Unaona, unabatizwa katika Jina la Yesu Kristo, naam, bwana, ukaingizwa katika ushirika; bali unabatizwa kwa Roho Mtakatifu, ukaingizwa ndani ya Yesu Kristo. Kwa hiyo unaweza ukabatizwa mara mia moja vyo vyote ambavyo ungetaka, vinginevyo, haingeleta tofauti yo yote. Lakini mara unapokuwa umebatizwa na Roho Mtakatifu, ukaingizwa katika Mwili wa Kristo, unakuwa mwana ama binti wa Mungu, na, "Kila Neno ni kweli!" Na, basi, Yeye alifanya jambo hilo kwa kusudi hilo.

221 Kama nilivyosema hivi majuzi, wakati Mungu alipotenda kazi na kuangaza jua kote duniani, Yeye alijua hiyo mitende na kila kitu vilikuwa viko pale chini ya hiyo ardhi. Yeye. . . Ilikuwa ni sehemu ya dunia wakati huo, na wewe vivyo hivyo.

222 Na wakati Yeye alipomfufua Mwana wa Mungu, kwenye asubuhi ya Pasaka, kisha akamtuma Roho Mtakatifu, ilikuwa ni kwa ajili ya kuhuisha, pia, ile mbegu ya Uzima wa Milele, ambayo alitangulia kuijua kabla ya kuwekwa msingi wa ulimwengu, kwamba ingekuwapo hapa. Yeye alijua maikrofoni hii ingefanya hivi jioni ya leo. Alijua ya kwamba wewe ungekuwa na msimamo ulio nao. Yeye hana kikomo. Huwezi kuliwazia kwa akili zako, inakubidi tu kulikubali. Lakini, hebu niseme jambo hili moja. Mungu yuyo huyo amesimama hapa, alasiri ya leo, ndani ya watu Wake.

223 Kwamba wewe ni Mmethodisti, Mbaptisti, Mpentekoste, cho chote ambacho ungekuwa, usitegemee madhehebu fulani. Maana, hao hawawezi kuwa madhehebu . . . Yana chungu mbovu ya mafundisho mbalimbali. Yana hao. . . Inakupasa kuwa mtu binafsi, kwa Mungu. Inakupasa kuwa mtu binafsi. Mungu hushughulika na wewe, si katika kanisa lako. Inakupasa kuishi maisha yaliyo mema kanisani mwako ama kwenye kusanyiko lako ambako unaabudia, unapaswa kuishi maisha ya namna hiyo unayopaswa kuwa. Lakini unaona, wao wanaunda kanuni za imani, na kadhalika, hivi kwamba hata huwezi kuingia kwenye milango yao kama huamini hayo. Kwa hiyo Mungu anawezaje kuingia humo, wakati Neno Lake linadhihirishwa daima?

224 Luther alijuaje juu ya ubatizo huu na—na kurudishwa kwa Roho, wakati akiwa aliishi huko nyuma kwenye siku zile? Mmea haukuwa umekua namna hiyo. Wala Wesley hakujua hilo.

Na wala Wapentekoste hawajui kile kinachoendelea siku hizi. Jambo lile lile, unakua moja kwa moja bila ya wewe kujua. Hiyo ni kweli. Limefanya hivyo katika kila wakati, na daima litakuwa.

225 Nami ninaweza kuthibitisha, kwa Biblia, huu ni wakati wa ngano. Kumbukeni, baada ya uamsho huu mkuu . . . Hapajatokea madhehebu mengine tangu Pentekoste. Hayawezi kuwapo. Inatoka kwenye kapi kwenda kwenye ngano, wala hakuna kitu kingine ila ngano. Hiyo ndiyo sababu. Miaka kumi na tano . . . Kwa kawaida, miaka mitatu, tayari wameunda madhehebu baada ya ufufuo wo wote. Mwulize mwanahistoria ye yote. Bali hakuna madhehebu baada ya Huu. Walijaribu kuunda moja la Mvua ya Vuli, bali mnaona kilicholipata. Haiwezekani. Ni ngano sasa. Naam, bwana. Hakuna wabebaji tena. Ni ngano halisi. Kristo yuko miongoni mwa watu Wake. Mnaamini jambo hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

226 Hebu na tuanzie kutoka *hapa*, kwenye sakafu ya chini. Siwezi kuita kutoka huko, kwa kuwa mko wengi sana. Ni wangapi wanaoamini mimi ni mtumishi Wake? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Iweni na imani kwa Mungu! Ni wangapi upande *huu* wanaamini hilo vivyo hivyo, semeni, "Ninaamini jambo hilo kwa moyo wangu wote"? ["Amina."] Sasa Bwana Mungu na atujalie jambo hili, ili mpate kuona zile nguvu za kuhuisha. Ni kitu fulani, ushahidi muhimu unaothibitisha hilo.

227 Naam, mtu fulani aweza aseme, "Loo, *hili* ni Lile, *hili*, *lile*." Bali hebu acha litende kazi.

228 Sasa, haiwezekani kabisa kwangu mimi kujua jambo lo lote kukuhusu wewe. Unajua hilo. Sina nimjuaye ila mtu mmoja tu, ninayeweza kumwangalia, na huyo ni Kasisi Blair aliyeketi pale, anayetoka huko mbali mashariki, ninaamini ni huko Arkansas ama mahali fulani huko mbali. Huyo ndiye mtu pekee katika wasikilizaji, ambaye ninaona kwamba ninamjua. Na Mungu anajua hilo ni kweli. Kwa hiyo itabidi iwe ni kitu ambacho . . .

229 Imetokea tu kwamba nimemwona hapa, maskini bibi huyu anayeketi pale mwisho, ana shida ya kiroho unayoiombea. Je! unaamini ya kwamba Mungu ataiweka sawa hiyo shida yako ya kiroho, na kuitatua? Vema, unaweza kulipokea.

230 Weka mkono wako juu ya huyo bibi mwingine anayeketi karibu nawe, maana yeye ana matatizo ya tumbo anayoombea, pia. Naam. Hiyo ni kweli, dada? Inua mikono yako kama hiyo ni kweli. Mimi siwajui, sijawaona kamwe maishani mwangu. Wasichana wawili weusi.

231 Sasa, hicho ni kitu gani? Je! hilo silo hasa kama lile alilosema Yeye angefanya? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Ni vile vile kabisa.

232 Huyu hapa bibi mmoja ameketi, akiangalia moja kwa moja kupitia hapa chini; ameketi, akiniangalia. Ana matatizo ya moyo. Je! unaamini ya kwamba Mungu ataponya hiyo shida ya moyo? Ulikuwa umeketi pale ukiomba, "Laiti ningaliweza kufika pale." Hiyo ni kweli? Tikisa mkono wako namna *hii*, ni kweli. Nilijuaje uliyokuwa ukisema katika maombi yako?

Unaona, amini tu. Ni hayo tu yanayokubidi kufanya, ni kuamini.

233 Huyu hapa bibi anayeketi hapa ambaye atakufa sasa hivi kama hataponywa. Ana kansa. Je! unaamini ya kwamba Mungu ataponya hiyo kansa? Naam. Unaamini hilo? Wewe, kwa kuwa kwa namna fulani ulichelewa kuinua mkono wako, je! unaamini Mungu anaweza kuniambia wewe u nani? Bi. Gunn. Sasa, kama hiyo ni kweli, tikisa mkono wako namna *hiyo*, unaona. Sawa. Nenda nyumbani, Yesu Kristo atakuponya.

"Kama unaweza kuamini, mambo yote yanawezekana."

234 Hilo lilimgusa bibi huyu anayeketi pale amevaa kofia nyeusi, akiniangalia. Yeye pia ana kansa. Je! unaamini Mungu atakuponya? Je! unaamini hayo kwa moyo wako wote? Ninazungumza na Bibi Miller. Je! unaamini hilo? Simjui mwanamke huyu, sijapata kumwona maishani mwangu, na Mungu Mbinguni anajua hiyo ni kweli. Amina.

"Kama unaweza kuamini!"

235 Hapa pana mwanamke mweusi ameketi hapa mwisho kabisa, alikuwa ameinamisha kichwa chake. Alikuwa akiangalia kwa makini, anachunguza kwa makini kwa ajili ya mpenzi wake, mtu fulani ambaye yeye anaombea. Alikuja, kwa kweli, kuomba . . . kusudi aombewe. La yeye hayuko hapa, ni mumewe. Hiyo ni kweli. Huyu mama . . . Mumewe hayuko hapa. Yuko nyumbani. Amefanyiwa upasuaji, sivyo? Hiyo ni kweli. Alikuwa akisumbuliwa na uvimbe wa puani, na kadhalika. Hiyo ni kweli, sivyo? Atapona. Imani yako ilikuwa na nguvu kwa ajili ya hilo. Unaamini ya kwamba hilo ni la kweli? Amina.

236 Hivi hamwezi kuona ya kwamba Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele? Waulizeni watu hao. Ameenda moja kwa moja upande mwingine wa wasikilizaji. Je! unaamini ya kwamba Yeye yuko hapa? Je! unahisi zile nguvu za kuhuisha ndani yako? Sawa, huyo ndiye Mungu anayewafanya wazima, enyi wapendwa. Mnaamini jambo hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

237 Sasa je! mtanitendea jambo moja? Kwa kuwa, ni wangapi waliopo hapa ndani ambao ni wagonjwa, hebu nione ukiinua mkono wako. Sasa inaelekea kwenye saa kumi na moja. Wekeaneni mikono ninyi kwa ninyi, na hebu tuninii tu . . . Msiseme neno sasa, wekeaneni tu mikono yenu mmoja—mmoja kwa mwingine. Ninawatakeni mfanye jambo fulani.

238 Aisee, mtu anayeketi papa hapa nyuma, ana ule uvimbe mgongoni mwake. Je! unaamini ya kwamba Mungu ataondoa uvimbe huo mgongoni mwako, bwana? Unaamini ya kwamba Mungu atakuponya? Ewe kijana, unayeniangalia, na akafikiri atapitwa. Inua mkono wako, bwana. Hiyo ni kweli. Amini kwa moyo wako wote, Mungu atakuondolea huo.

239 Haleluya! Ninawasai wasikilizaji hawa wote, katika Jina la Yesu Kristo! Kama mngeweza, kama. . . Dhamira yako, usiache iunguzwe kwa chuma cha moto wa kutokuamini, usiache ifadhaishwe. Hivi huwezi kumwona Mwana wa Adamu, Mwana wa Adamu katika mfano wa Ujumbe wa kinabii, akirudi tena katika Kanisa Lake, katika unabii, akimfunua Yesu Kristo kwamba ni yeye yule jana, leo, na hata milele? Halijawahi kufanyika kote katika wakati huu, mpaka kufikia saa hii. Unaona? Hilo hapo thibitisho lake.

240 Kanisa ni kitu gani? Unaingiaje humo? Unapokuwa humo ndani, kila kitu alichokuwa Yesu Kristo, ndicho ulicho, hata kuwa mwana na binti wa Mungu. Yeye alifanyika wewe nawe upate kufanyika Yeye.

241 Jambo lenyewe ni kwamba, unaogopa kuitumia hiyo, la sivyo hushirikiani na Neno Lake. Sasa, hilo halitafaa kitu, wala si—sijali utakalofanya. Usipoingia kikamilifu katika Neno hilo, halitafaa kitu kamwe. Ni nani anayeweza kunisema kuhusu jambo ambalo Yeye alisema na kuliahidi kwa siku hii, ambalo halikutukia? Basi usinitupie madhehebu yako, maana hayatafanya cho chote.

242 Haleluya! Ninajisikia, ninajua Yeye yuko hapa. Nina hakika Yeye yuko hapa. Ninajua ya kwamba sasa kuna nguvu za kuhuisha ndani ya Kanisa kumponya kila mtu anayeketi hapa. Je! mnaweza kuamini jambo hilo? Vema, basi, hivi mtaamini?

243 Je! mnaamini katika kuwaombea wagonjwa? Mnaamini Yesu alisema, "Wataweka mikono yao juu ya wagonjwa, nao watapata afya"? Sawa, wekeaneni mikono sasa. Usijiombee. Mwombeeni mtu huyo mwingine karibu yako. Wao wanakuombea. Sasa polepole na kwa uchaji.

244 Bwana, jinsi ninavyokushukuru, ninaweza kusimama hapa kwenye jukwaa hili na—na kuhubiri Neno ambalo liko kinyume sana na mawazo ya watu katika siku hizi, hivi kwamba wangeliliita Hilo ni "uzushi," wangeliliita "umizimu," wangeliliita "pepo wachafu," kama walivyofanya, wakati huo, "Beelzebuli." Bali kukuona Wewe moja kwa moja katikati ya wasikilizaji hawa wapendezao, alasiri ya leo, ukigeuka moja kwa moja na kuthibitisha na kubainisha yale hasa yaliyohubiriwa, kwamba Hiyo ni Kweli.

245 Mungu, hawa ni watu Wako. I—Ibilisi amejaribu kuvuruga maikrofoni, amejaribu kuvuruga mawazo ya watu, amejaribu kuwafanya wasiupate Huu. Lakini ninaamini wataupata, hata

hivyo, Bwana. Ninaomba kwamba waupate. Ninaomba kwamba waupokee. Tujalie, Bwana, hawa waamini walio na nguvu za kuhuisha, ya kwamba wakati wao. . . wasipoishi kuona Kuja Kwako, nguvu hizo za kuhuisha zitawafufua katika siku za mwisho.

246 Jalia sasa ya kwamba nguvu hizo za kuhuisha zitaihuisha imani yao, Bwana, kwa yale wanayofanya. Kuna mwamini aliyeweka mikono yake juu ya mwamini, mwili kwa mwili, nguvu kwa nguvu. Na ni nguvu za Mungu, kwa mwana wa Mungu ama binti ya Mungu, kwa Mwana wa Mungu. Ee Mungu, jalia Shetani awaachilie watu hawa! Jalia waponywe alasiri ya leo, kwa nguvu hizo za kufufuka, kuhuisha kwa Uwepo uliotambulishwa, Yesu Kristo. Katika Jina la Yesu Kristo, na iwe hivyo!

247 Mikono yenu juu ya hao watu ina nguvu za kuhuisha ndani yao, kama umekwisha kuhuishwa. Je! umeingia Uzimani? Je! Kristo amekuwa halisi kwako? Je! nguvu za Mungu zimedhihirishwa? Je, wewe uko ndani ya lile Kanisa, Kanisa lililoletwa na Mungu? Unakuwaje ndani Yake, unajuaje umehuishwa ndani Yake? Mawazo yako yote, utu wako wote, umo ndani ya Kristo sasa. Naye Kristo yuko miongoni mwa watu, akijithibitisha kwamba yu hai, akithbitisha ya kwamba Yeye yuko hapa kwenye siku za Sodoma.

248 Pamoja na mikono ya watu hao, ya kwamba maisha yao yamebadilishwa toka wazururaji wa mitaani, toka walevi, toka makahaba mtaani, kuwa watakatifu halisi wa Mungu, waliohuishwa. Mikono yao imewekwa juu yako. Wamo ndani ya lile Kanisa, kwa ubatizo wa Roho Mtakatifu, nguvu zile zile zilizokuwa juu ya mifupa ya Eliya. Nguvu zizo hizo zimekaa mabegani mwako, juu ya mikono yako, juu ya vichwa vyenu, nguvu zizo hizo za kuhuisha; huku Yeye akiwa amesimama hapa akithibitisha ya kwamba Yeye amefufuka toka kwa wafu, anajionyesha Mwenyewe kwamba yu hai, yuko hapa sasa akifanya mambo yale yale aliyofanya wakati alipokuwa. . .?. . . Amina!

249 Je! unaweza kumwamini sasa? Je! unaweza kuamini ya kwamba mikono hiyo iliyowekwa juu yako ni mikono ya kiungu, je! unaweza kuamini Roho hiyo inayotuhuisha sasa, inayotufanya tutende kiwenda wazimu kwa ulimwengu, je! unaamini hizo ni nguvu Zake za kuhuisha? Je! unaamini uko ndani ya Kanisa Lake? Basi, kama uko humo, na unaamini ya kwamba mikono hiyo uliyowekewa ni mikono mitakatifu, iliyoagizwa na Mungu; basi ninakuamuru, katika Jina la Yesu Kristo, kusimama kwa miguu yako na ukubali uponyaji wako, kila mtu ambaye alikuwa ni mgonjwa.

Loo, ewe Mkristo, unatambua ni jambo gani limetukia?

250 Je! Unatambua, huko kwenye ile barabara ile kule ng'ambo kuna mamilioni ya watu wanaotembea kwenye barabara hizi, leo, ambao si si cho chote bali ni chakula cha atomiki? Je! unatambua watu hao wamekufa katika dhambi na makosa, na maisha ni meusi; makanisani kila mahali, kwa ajili ya mihadhara michache ama cho chote kile kuhusu kutimiza jambo fulani, na kukiita dini.

251 Je! hivi ulitambua ya kwamba umekwishafufuliwa kutoka mautini kuingia Uzimani, na umekwisha kubatizwa katika Mwili wa Mungu aliye hai ambaye ameihuisha miili yenu, palipo na kunena kwa lugha na kutafsiri lugha, kumwona Yesu Kristo amedhihirishwa miongoni mwetu? Mbona, ugonjwa usingeweza kusimama katika kundi kama hili. Achilia imani yako na imwendee Yeye, umwamini Yeye! Useme, "Bwana Mungu, ninaamini kwa moyo wangu wote," nawe utakuwa mzima.

252 Je! kuna wenye dhambi hapa ambao wangetaka kuingia katika Mwili huo? Inueni mikono yenu, na mseme, "Sijapata kuingia Humo, sijawahi kujazwa na Roho Mtakatifu, lakini, Ndugu Branham, hakika ninamtamani alasiri ya leo. Je! utaniombea?" Inueni mikono yenu. Msione aibu, mko katika Uwepo Wake. Hebu iangalieni tu mikono hiyo! Hebu iangalieni tu mikono hiyo!

253 Sasa kila mtu anayetaka ubatizo wa Roho Mtakatifu, inueni mikono yenu, po pote mlipo, wanaoutaka.

254 Sasa ninyi mlio na Roho Mtakatifu, mnaosimama karibu nao, wekeni mikono yenu mitakatifu, iliyowekwa wakfu juu yao. "Ikiwa Roho Mtakatifu, aliyemfufua Yesu katika wafu, anakaa ndani yenu, anaihuisha miili yenu, kutoka mautini kuingia Uzimani." Anauleta mwili wote chini ya mamlaka ya Roho. Sasa hebu na tuinamishishe vichwa vyetu, na kila mtu na awaombee hao watu wanaotaka ubatizo wa Roho Mtakatifu. Nami ninaamini ya kwamba Mungu atamjaza kila mmoja wenu, sasa hivi, na Roho Mtakatifu.

255 Kwa nini tungojee, enyi wapendwa? utangojea mno kupita kiasi, moja ya siku hizi. Hii ndiyo ile saa. Usingoje zaidi. Uko papa hapa katika hekalu hili ambapo una usiku mzima wa kukaa na kuomba.

256 Mungu mpenzi, ninaomba ya kwamba Wewe utamtuma Roho Mtakatifu tena, kama vile upepo wenye nguvu ukienda kasi, aijaze nyumba hii yote, baada ya huu utambulisho mkamilifu hapa, alasiri ya leo, kwamba Wewe uko hai na uko pamoja na watu hawa. Katika Jina la Yesu. Amina.

*Mahali Pa Kuabudia Palipoandaliwa Na Mungu* SWA65-0425
(God's Provided Place Of Worship)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, ulitolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumapili alasiri, tarehe 25 Aprili, 1965, katika Embassy Hotel kule, Los Angeles, California, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice of God Recordings.

SWAHILI

©2007 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

# Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

Voice Of God Recordings
P.O. Box 950, Jeffersonville, Indiana 47131 U.S.A.
www.branham.org